Haliuzwi

AGOSTI 25, 2026
/islamicftz
Rabi ul-Awwal 12 1448

IMAAN

ISSN 5618 - NO. 595

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

SHEIKH TWAHA: Wazazi, shule shirikianeni kujenga maadili ya watoto

KAMBI YA MATIBABU YA MACHO

Zaidi ya 300 wafanyiwa upasuaji bure Kondoa

- 2,500 wapewa miwani
- Waziri Kijaji aimwagia sifa Al-Muntada, The Islamic Foundation

Sukuk Afrika dola bilioni 7, Misri yashikilia karibu nusu

Tanzania yaja na umeme wa kuuza

"Rais Samia Suluhu Hassan akizindua Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Julius Nyerere ambapo aliagiza nguvu ielekezwe katika kuuza umeme nje ya nchi. Mradi huo umepandisha uwezo wa kuzalisha umeme nchini kufikia megawati 4,646 (MW) ikilinganishwa na mahitaji ya juu ya megawati 2,271, hivyo kuwa na ziada ya takribani MW 2,375.

Z'bar yalenga Wasaudi Arabia kwa utalii halal

- Yafungua pia fursa za mafuta, gesi, nishati na uchumi wa buluu

Ukifa, unaacha nini kama Waqf?

Machafuko Afrika Kusini, Serikali yawarejesha Watanzania 669

NA MWANDISHI WETU, KONDOA

KAMBI YA MATIBABU YA MACHO

Zaidi ya 300 wafanyiwa upasuaji bure Kondoa

Wananchi 301 wa Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma wamefanyiwa upasuaji wa macho bila malipo, huku 1,859 wakipatiwa miwani kupitia kambi maalumu iliyoratibiwa na Taasisi ya The Islamic Foundation kwa ufadhili wa Shirika la Al-Muntada Aid la Uingereza.

Kambi hiyo iliyofanyika Agosti 20 hadi 23, 2026 katika vituo vya Pahi na Bukulu, iliwafikia maelfu ya wananchi kwa huduma za uchunguzi, matibabu, miwani na upasuaji wa macho.

Katibu Mkuu wa The Islamic Foundation, Musa Buluki, alisema katika kituo cha Pahi pekee wagonjwa 106 walibainika kuhitaji upasuaji, huku zaidi ya wagonjwa 270 wakifanyiwa upasuaji katika vituo vyote viwili.

Alisema huduma hizo zimewapunguzia wananchi mzigo wa gharama za matibabu na usafiri, hasa familia zenye uwezo mdogo ambazo hulazimika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za kibingwa.

Katika kufanikisha kampeni hiyo, Buluki alisifu ushirikiano kati ya The Islamic Foundation, Al–Muntada Aid na wadau wa eneo hilo, wakiwemo viongozi, uliowawezesha huduma hizo kuwafikia wananchi wengi kwa wakati, akisisitiza umuhimu wa kuendelea kuandaa kambi kama hizo katika maeneo mengine yenye uhitaji mkubwa.

Akizungumza na Gazeti Imaan katika kambi hiyo, Mbunge wa Kondoa Vijijini na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Ashatu Kijaji, aliishukuru Al-Muntada Aid na The Islamic Foundation kwa kuwafikishia wananchi huduma hizo.

"Wananchi wengi wamekuwa wakifika katika ofisi yangu kuomba msaada wa matibabu, nauli, dawa na hata gharama za upasuaji. Kambi hii imewasaidia kupata huduma karibu na maeneo yao na kupunguza gharama ambazo wangetumia kusafiri," alisema.

Waziri asifu, ashukuru

Dkt. Kijaji alisema The Islamic Foundation imekuwa sehemu ya juhudi za kuwasaidia wananchi wenye changamoto mbalimbali, hususan wale wanaohitaji matibabu lakini hawana uwezo wa kumudu gharama.

Aliomba ushirikiano huo uendelezwe na kuishauri The Islamic Foundation pamoja na wafadhili wengine kuangalia uwezekano wa kuandaa pia kambi ya matibabu ya magonjwa ya ngozi, akisema baadhi ya wananchi hulazimika kusafiri hadi vituo kama KCMC kupata huduma hizo.

Mbunge huyo pia aliwasihi wananchi waliofanyiwa upasuaji kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya, kutumia dawa kwa usahihi na kuzingatia masharti yote ya matibabu ili kuhakikisha wanapata nafuu na kurejea katika shughuli zao za kila siku wakiwa salama.

Kauli za wadau wengine

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Soera, ambako kambi hiyo ilifanyika amemshukuru Dkt. Kijaji pamoja na Taasisi ya The Islamic Foundation kwa kuwafikishia wananchi huduma hiyo.

Alisema hatua ya Taasisi ya The Islamic Foundation kutoa huduma za matibabu ya macho bila malipo inaendana na dhana ya Serikali ya Awamu ya Sita ya "Kazi na Utu."

Naye kiongozi wa timu ya watu waliojitolea kufanikisha kambi hiyo, inayojulikana kama TIF Volunteers, Sheikh Muhammad Juma, amesema zoezi hilo limefanikiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na ushirikiano mkubwa kutoka kwa wananchi wa Kondoa.

Sheikh Juma aliwapongeza wananchi hao kwa ukarimu na utulivu waliouonesha wakati wote wa zoezi hilo, na kukubalian na utaratibu wa kuwapa kipaumbele wagonjwa waliokuwa na mahitaji makubwa na hivyo zoezi kwenda kwa ufanisi.

ربيع أوّل

HABARI

NA MWANDISHI WETU

RUFIJI

Kutoka uhaba wa umeme hadi kuuza umeme nje ya nchi

■ **Tanzania inaelekea kuanza kuuza ziada ya umeme ya MW 2,375 katika masoko ya kikanda, ikilenga Zambia, Kenya na DRC, huku miundombinu mipya ya usafirishaji ikiimarisha azma ya kuugeuza umeme kuwa chanzo cha mapato ya fedha za kigeni**

4,646
Megawatt
Uwezo wa uzalishaji umeme uliowekwa

2,271
Megawatt
MW za mahitaji ya juu ya umeme nchini

2,375
Megawatt
Ziada ya makadirio ya uzalishaji: MW 2,375

MAUZO KWA ZAMBIA: MW 1,000

Serikali imekamilisha mazungumzo ya kuuza megawati 1,000 za umeme kwa Zambia. Masoko mengine yanayojadiliwa ni Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Serikali imeanza kuelekeza nguvu katika kuuza umeme nje ya nchi baada ya kukamilika kwa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP), uliopandisha uwezo wa uzalishaji wa taifa hadi kufikia kiwango kikubwa kuliko mahitaji ya juu ya matumizi ya ndani.

Waziri wa Nishati, Deogratius Ndejembi, alisema Jumamosi kuwa uwezo wa kuzalisha umeme nchini umefikia megawati 4,646 (MW), ikilinganishwa na mahitaji ya juu ya megawati 2,271, hivyo kuwa na ziada ya takribani MW 2,375.

Hatua hiyo imeibadilisha Tanzania kutoka taifa lililokuwa likikabili changamoto ya upatikanaji wa umeme na sasa kuanza kutafuta masoko ya kikanda kwa ajili ya kuuza nishati hiyo kwa nchi jirani.

Serikali tayari inafanya mazungumzo na Zambia, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), huku Tanzania ikiwa mwanachama wa Eastern Africa Power Pool (EAPP) na Southern African Power Pool (SAPP), jambo linaloiunganisha na masoko mapana ya umeme katika kanda hizo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa JNHPP uliopo Rufiji, mkoani Pwani, Ndejembi alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza umeme usichukuliwe kama huduma ya umma pekee, bali pia bidhaa inayoweza kuuzwa na kuingiza fedha nchini.

Alisema Tanzania imekamilisha mazungumzo na Zambia kuhusu uuzaji wa MW 1,000, huku mazungumzo na nchi nyingine yakiendelea.

Mkakati huo unatarajiwa kuongeza mapato ya fedha za kigeni na kutoa nafasi ya kuwekeza zaidi katika uzalishaji na usafirishaji wa umeme.

JNHPP ina mitambo tisa ya kuzalisha umeme, kila mmoja ukiwa na uwezo wa MW 265, hivyo kuwa na uwezo wa jumla wa MW 2,115.

MATUKIO KATIKA PICHA

Na Ikulu

Rais Samia Suluhu Hassan amezindua Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Julius Nyerere, ndoto ya miaka mingi ya MW 2,115

> "Tuna imani kwamba mradi huu utaongeza fursa za biashara, uwekezaji, uzalishaji, kutengeneza ajira na kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na pato la Taifa kwa ujumla."
>
> *Rais Samia Suluhu Hassan*

NA MWANDISHI WETU

SAFARI YA KUSAKA UKWELI

Siku 150 za Tume kuwasaka wapanga, wafadhili wa vurugu zaanza rasmi

■ Tume ya Jaji Lila kazini rasmi, kuchunguza vifo 518, matumizi ya silaha za moto na nguvu kupita kiasi. Wahusika wote kufikiwa wakihitajika, uwazi, usiri kuguswa.

Tume ya Uchunguzi iliyoundwa kuchunguza waliohusika na vurugu pamoja na madai ya ukiukwaji wa sheria wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025, imeanza rasmi kukusanya ushahidi, ikiwa imepewa siku 150 kukamilisha kazi hiyo.

Tume hiyo yenye wajumbe sita, ikiongozwa na Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Shaban Ally Lila, imeanza kazi yake ya uwandani Jumatatu katika Wilaya ya Kigamboni, Dar es Salaam, kabla ya kuelekea maeneo mengine yanayohusishwa na matukio yanayochunguzwa.

Mwanzo wa kazi hiyo unaashiria hatua mpya ya uchunguzi unaolenga kubaini watu waliopanga, kufadhili, kuratibu au kushiriki katika vurugu hizo, pamoja na kuchunguza madai ya vifo, majeruhi, watu kupotea na ukiukwaji mwingine wa sheria uliodaiwa kutokea wakati na baada ya uchaguzi.

Tume hiyo ilianzishwa na Rais Samia Suluhu Hassan kufuatia mapendekezo ya Tume ya awali iliyoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu, Mohamed Chande Othman.

Akizungumza wakati wa kuanza kwa kazi hiyo, Jaji Lila alisema tume yake itafanya uchunguzi wa kina kuhusu masuala yaliyobainishwa na tume iliyotangulia na kutumia njia mbalimbali kupata taarifa sahihi.

Alisema ushahidi utakaokusanywa utajumuisha ushahidi wa moja kwa moja kutoka kwa mashahidi, nyaraka pamoja na taarifa zitakazopatikana wakati wajumbe watakapotembelea maeneo ambako matukio yalitokea.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, tume itatembelea maeneo yote yanayohusiana na matukio yaliyo ndani ya hadidu za rejea, huku ikichunguza madai ya watu waliopanga, kufadhili, kuratibu na kutekeleza vurugu.

Pia itachunguza matukio maalumu yaliyoibuka wakati wa juhudi za kudhibiti vurugu, ikiwamo madai ya vifo visivyo vya kawaida vya watoto na watu waliokuwa katika makundi hatarishi.

Masuala mengine yatakayochunguzwa ni madai ya watu kupata majeraha makubwa kutokana na matumizi yasiyo halali ya silaha za moto, watu kupigwa risasi nje ya maeneo yaliyokuwa yamekumbwa na vurugu na taarifa za watu waliopotea wakati na baada ya uchaguzi.

Tume pia itachunguza madai ya matumizi ya nguvu kupita kiasi, kinyume na sheria, taratibu na miongozo iliyowekwa wakati mamlaka zilipokuwa zikidhibiti vurugu hizo.

Jaji Lila alisema tume itazingatia pia jambo lolote litakaloonekana kuwa muhimu kwa utekelezaji wa hadidu zake za rejea.

Majaji wa kigeni waingia kazini

Uchunguzi huo pia unahusisha majaji wawili kutoka nje ya Tanzania, ambao ni Naibu Jaji Mkuu wa Namibia, Petrus Tileinge Damaseb, na Jaji wa Mahakama ya Rufani Uganda, Barishaki Bonny Cheborion.

Ushiriki wao unalenga kuongeza uzoefu wa kimahakama na mtazamo wa kikanda katika uchunguzi huo.

Jaji Damaseb alisema atatumia uzoefu wake wa kimahakama kuchangia kazi hiyo, akisisitiza umuhimu wa uhuru wa tume.

Kwa upande wake, Jaji Cheborion alisema atatumia uwezo na uzoefu wake kuhakikisha tume inakamilisha jukumu lake kwa mafanikio.

Alikumbusha uhusiano wa muda mrefu kati ya Tanzania na Uganda, akisema Tanzania iliisaidia Uganda wakati wa utawala wa Idi Amin Dada na kwamba sasa ni wakati wa Uganda kuchangia kwa Tanzania.

Tume yaahidi uhuru

Jaji Lila pia amesisitiza kuwa tume itafanya kazi kwa uhuru ndani ya sheria, akisema jukumu la Rais ni kuwateua wajumbe na kuweka hadidu za rejea, si kuelekeza namna uchunguzi unavyopaswa kufanywa.

NA MWANDISHI WETU

Zanzibar kutumia utalii halal kuvutia wawekezaji kutoka Saudi Arabia

Yafungua pia fursa za mafuta, gesi, nishati na uchumi wa buluu

Zanzibar ambayo imeanza kutekeleza Sera ya Utalii Halal inapambana kuvutia zaidi watalii kutoka Saudi Arabia, hasa wanaosafiri pamoja na familia zao, sambamba na kufungua fursa mpya za uwekezaji kutoka taifa hilo.

Waziri wa Kazi na Uwekezaji, Shariff Ali Shariff, alisema hayo katika Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Zanzibar na Saudi Arabia lililofanyika Agosti 20, 2026.

Alisema Zanzibar imejiandaa kupokea wawekezaji, hususan kutoka Saudi Arabia, katika sekta ya utalii pamoja na uchumi wa buluu, kilimo, mafuta, gesi na nishati.

Kwa mujibu wake, utafiti wa mafuta na gesi unaendelea vizuri na unaonyesha matumaini, huku Zanzibar ikiwa pia na fursa katika uzalishaji wa nishati ya jua na upepo.

Kongamano hilo lilihudhuriwa na ujumbe wa wawekezaji na wafanyabiashara kutoka Saudi Arabia ulioongozwa na Balozi wa Tanzania nchini humo, Zena Saidi.

Balozi Zena alisema uwekezaji kutoka Saudi Arabia kwenda Zanzibar umekuwa mdogo, hivyo ziara hiyo inalenga kufungua ukurasa mpya wa ushirikiano wa kiuchumi.

"Tunataka sasa uwekezaji kutoka Saudi Arabia uongezeke. Wawekezaji hao wana hamasa kubwa, hasa katika masuala ya usalama wa chakula na nishati," alisema.

Alisema wawekezaji hao pia wanatafuta maeneo ya kilimo na fursa za kujenga matanki makubwa ya kuhifadhia mafuta kwa matumizi ya kawaida na wakati wa dharura.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Saleh Saad Mohamed, alisema baadhi ya wajumbe wameongeza muda wa kukaa Zanzibar ili kukagua maeneo ya uwekezaji.

Alitaja majengo na ardhi, teknolojia, usafirishaji na miundombinu muhimu kuwa miongoni mwa maeneo yanayowavutia wawekezaji hao.

MATUKIO KATIKA PICHA

Na Mpigapicha Wetu

Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Zanzibar na Saudi Arabia



NA MWANDISHI WETU, DODOMA

SHEIKH IBRAHIM TWAHA:

Wazazi, shule shirikianeni kujenga maadili ya watoto

Wazazi na walezi wametakiwa kuendeleza majumbani maadili ambayo watoto wanafundishwa shuleni ili elimu wanayopata iende sambamba na malezi yanayowajenga kuwa raia wema na wenye mchango chanya katika jamii.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi wa Taasisi ya The Islamic Foundation, Sheikh Ibrahim Twaha, wakati wa mahafali ya pili ya Shule ya Msingi Imaan, mkoani Dodoma iliyofanyika viwanja vya shule hiyo.

Sheikh Twaha alisema elimu inayotolewa shuleni inapaswa kwenda sambamba na malezi bora na ujenzi wa maadili, huku akisisitiza kuwa wazazi wana wajibu mkubwa wa kuhakikisha misingi inayowekwa kwa watoto shuleni inaendelezwa pia katika familia.

Katika hatua nyingine, aliahidi kutimiza ahadi ya kuipatia Shule ya Msingi Imaan kompyuta, hatua inayolenga kuongeza fursa za wanafunzi kupata elimu ya teknolojia na kuendana na mahitaji ya elimu ya kisasa.

Alisema pia wanafunzi watakaohitimu Shule ya Imaan na kujiunga na Sekondari ya Forest Hill watapewa kipaumbele pamoja na punguzo maalumu la ada, ili kuwawezesha kuendelea na elimu katika mazingira bora.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Imaan Dodoma, Dkt. Shadidu Ndossa, aliishukuru The Islamic Foundation, chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Aref Nahdi, kwa kutekeleza ahadi mbalimbali zilizotolewa mwaka uliopita na kuendelea kushirikiana na shule katika kuimarisha mazingira ya elimu.

Dkt. Ndossa alisema ushirikiano huo umechangia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, huku akiwataka wazazi kuendelea kushirikiana na walimu kuhakikisha watoto wanapata elimu bora pamoja na malezi yanayojenga nidhamu na maadili.

Naye Mkurugenzi wa The Islamic Foundation Mkoa wa Mwanza, Abdulhakim Abeid, aliupongenza uongozi wa Shule ya Imaan kwa usimamizi mzuri wa elimu.

Aliwahimiza wazazi kuwapeleka watoto wao katika shule zinazowajengea maadili mema, misingi imara ya elimu na imani ya dini.

ربيع أول

MATUKIO KATIKA PICHA

Na Mpigapicha Wetu

Mahafali ya pili ya Shule ya Msingi Imaan, mkoani Dodoma iliyofanyika viwanja vya shule hiyo

NA UKHTIFATIMA SS
0789 201 383

Machafuko Afrika Kusini, Serikali yawarejesha Watanzania 669

Tanzania imeanza mchakato wa kuwarejesha kwa hiari raia wake wanaoishi katika Jimbo la KwaZulu-Natal nchini Afrika Kusini, huku kundi la kwanza likitarajiwa kuondoka Agosti 26, 2026.

Taarifa iliyotolewa juzi na ubalozi wa Tanzania mjini Pretoria inaeleza kuwa Watanzania waliopo KwaZulu-Natal, hasa Durban, ambao wameonesha nia ya kurejea nchini watafanyiwa taratibu za kupata vibali vya urejeshwaji kwa hiari Agosti 25 na 26.

Safari ya kurejea Tanzania imepangwa kufanyika Agosti 26 kwa kutumia ndege ya Shirika la Ndege la Taifa la Tanzania (ATCL), itakayoondoka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa King Shaka, Durban.

Ubalozi umewataka Watanzania ambao tayari wamejiandikisha kwa ajili ya safari hiyo kuwa na subira wakati taratibu za maandalizi ya kurejea zikikamilishwa.

Aidha, Watanzania wenye vyeti vya kuomba hifadhi wametakiwa kubaki katika kituo maalumu cha usindikaji hadi taratibu za vibali vyao zitakapokamilika.

Suala hilo linawahusisha Watanzania wasio na pasipoti, waliopoteza au ambao pasipoti zao zimekwisha muda wake, pamoja na watoto waliozaliwa Afrika Kusini na wazazi Watanzania, miongoni mwa waombaji wengine wanaokidhi vigezo.

Kwa Watanzania watakaokamilisha taratibu bila kuwa na pasipoti, watapatiwa Hati za Dharura za Kusafiria (ETDs) zitakazowawezesha kurejea Tanzania.

Kituo cha usindikaji kitakuwa City View Mall, 10 Mathews Meyiwa Road, Greyville, Durban, na kitafunguliwa kuanzia saa 12:00 asubuhi.

Ubalozi umewataka waombaji wanaohusika na suala hilo kufika kituoni kwa wakati na kufuata maelekezo yatakayotolewa wakati wa mchakato huo.

Mwishoni mwa Juni mwaka huu, hali ya taharuki iliendelea kutanda nchini Afrika Kusini huku maelfu ya wahamiaji wakianza kurejea katika nchi zao za asili kutokana na hofu ya kuongezeka kwa mashambulizi na maandamano ya kupinga wahamiaji yaliyopangwa kufanyika Juni 30.

Taarifa za vyombo vya habari nchini Afrika

UKHTI FATIMA SS

Sukuk Afrika dola bilioni 7, Misri yashikilia karibu nusu

Thamani ya sukuk zilizopo sokoni barani Afrika imevuka dola bilioni 7 hadi Agosti 2026, ikiwa ni ongezeko la takribani asilimia 16 ndani ya mwaka mmoja, huku Misri pekee ikishikilia karibu nusu ya soko hilo.

Kwa mujibu wa Fitch Ratings, Misri ina asilimia 48 ya sukuk zote za Afrika, ikifuatiwa na Nigeria yenye asilimia 26, Afrika Kusini asilimia 15 na Benin asilimia 7.

Misri imeongeza nafasi yake baada ya kuanza kutoa sukuk ya serikali ya dola mwaka 2023, kufuatia maboresho ya kanuni na kuimarika kwa uhusiano wa kiuchumi na nchi za Ghuba. Mwaka 2025 ilitoa sukuk yake ya kwanza ya fedha za ndani na kuendelea na utoaji katika nusu ya kwanza ya 2026.

Fitch imesema sukuk zinaibuka kuwa chanzo mbadala cha fedha kwa serikali za Afrika, zikiwawezesha kupanua vyanzo vya mitaji na kuvutia benki za Kiislamu, mifuko inayofuata Shariah na wawekezaji kutoka Ghuba.

Hata hivyo, ukuaji huo bado umejikita katika nchi chache. Afrika inachangia chini ya asilimia moja ya sukuk zote duniani.

Takribani dola bilioni 1 za sukuk zimetolewa Afrika mwaka huu hadi sasa, ikilinganishwa na dola bilioni 3.3 mwaka mzima wa 2025.

Fitch imetaja ukosefu wa mifumo rafiki ya kisheria na udogo wa taasisi za fedha za Kiislamu katika nchi nyingi kuwa miongoni mwa vikwazo vikubwa vya ukuaji wa soko hilo.



HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU

UKHTI FATIMA SS

Ethiopia yaongeza kasi huduma za fedha zisizo na riba

Ethiopia imeongeza kasi ya kukuza huduma za kifedha zisizo na riba kwa kuimarisha kanuni, teknolojia na utaalamu, hatua inayolenga kupanua ujumuishaji wa kifedha na kufikia wananchi ambao bado wako nje ya mfumo rasmi wa fedha.

Benki Kuu ya Ethiopia (NBE) imesema inaendelea kuboresha mifumo ya udhibiti wa benki zisizo na riba na Takaful, ikizitaja huduma hizo kuwa sehemu muhimu ya mkakati wa kuongeza ujumuishaji wa kifedha.

Benki hiyo pia inalenga kutumia maendeleo ya soko la mitaji na Soko la Hisa la Ethiopia kupanua fursa za huduma za fedha.

Hatua hiyo ilijadiliwa katika Kongamano la Sita la Kimataifa la Benki Isiyo na Riba na Takaful, lililofanyika Addis Ababa Agosti 17, 2026, likihusisha wadhibiti, wataalamu wa Shariah, kampuni za teknolojia na washiriki kutoka nchi 20.

Sekta hiyo hata hivyo inakabiliwa na upungufu wa wataalamu wenye ujuzi maalumu, ingawa takribani wataalamu 800 wa fedha nchini humo wamejiandikisha katika programu ya mafunzo ya fedha zisizo na riba mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Digaf Microcredit Provider imeingia ubia na AlHuda Centre of Islamic Banking and Economics kuanzisha huduma za mikopo midogo ya kidijitali isiyo na riba. Kupitia ushirikiano huo, Digaf inapanga kuanzisha kitengo maalumu cha fedha zisizo na riba, huku AlHuda CIBE ikitoa ushauri wa Shariah katika kuandaa bidhaa zinazolenga wajasiriamali, biashara ndogo na jamii ambazo hazijafikiwa vya kutosha na huduma rasmi za fedha.

Mambo safi mabadiliko benki Pakistan kuelekea Shariah

Pakistan imeongeza kasi ya kubadili mfumo wake wa benki za kawaida kuelekea mfumo unaofuata Shariah, huku sekta ya fedha za Kiislamu nchini humo ikitarajiwa kuvuka thamani ya dola bilioni 100 mwaka 2027.

Benki Kuu ya Pakistan imeunda kamati ya ngazi ya juu kusimamia mabadiliko hayo na kuongeza usimamizi wa ubadilishaji wa matawi ya benki za kawaida kuwa matawi ya Kiislamu.

Kwa mujibu wa Fitch Ratings, sehemu ya ufadhili inayotolewa na benki za Kiislamu ilifikia asilimia 38.2 mwishoni mwa robo ya kwanza ya 2026, kutoka asilimia 25.5 mwaka 2024.

Ukuaji huo umechangiwa kwa kiasi kikubwa na matawi ya Kiislamu yanayomilikiwa na benki za kawaida. Matawi hayo yalifikia asilimia 42.8 ya mali zote za taasisi za benki za Kiislamu, kutoka asilimia 34.4 mwaka 2024.

Sekta nzima ya fedha za Kiislamu Pakistan ilikuwa na thamani ya zaidi ya dola bilioni 90 kufikia nusu ya kwanza ya 2026. Benki za Kiislamu zilichangia asilimia 58 ya mali hizo, zikifuatiwa na sukuk asilimia 29.

Pakistan inalenga kuwa na mfumo wa fedha unaofuata Shariah kikamilifu ifikapo 2028.

Hata hivyo, Fitch imeonya kuwa kasi ya mabadiliko bado si sawa katika maeneo yote, huku sukuk, Takaful na taasisi za fedha zisizo za benki zikihitaji kukua kwa kasi zaidi ili kufikia lengo hilo.

Pakistan yatakiwa kuvuna fursa ya uchumi wa halal duniani

Pakistan ina nafasi kubwa ya kuongeza ushawishi wake katika uchumi wa halal duniani kwa kubuni bidhaa mpya za kifedha zinazofuata Shariah, kuboresha kanuni na kuongeza utaalamu, kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Islamic Chamber of Commerce and Development (ICCD), Yousef Hassan Khalawi.

Akizungumza katika mjadala wa Securities and Exchange Commission of Pakistan kuhusu fedha za Kiislamu, Khalawi alisema nchi hiyo inanufaika na idadi kubwa ya Waislamu, jumuiya kubwa ya raia walioko nje ya nchi na sekta inayokua ya fedha za Kiislamu.

Alisema Pakistan inapaswa kwenda zaidi ya huduma za kawaida za fedha za Kiislamu na kuwekeza katika maeneo kama teknolojia ya fedha, kilimo na mikopo isiyo na riba.

Khalawi pia alipendekeza mifumo ya uwekezaji inayotumia wakfu kukusanya hata michango midogo na kuielekeza katika miradi ya elimu, afya na miundombinu.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa viwango vinavyofanana vya Shariah na mafunzo maalumu kwa wataalamu ili sekta hiyo iweze kukua kwa ufanisi na kuhimili ushindani wa kimataifa.

NA MWANDISHI WETU

Wataalamu waonya kuitegemea AI kuamua hatima ya wanafunzi

Wito umetolewa Akili Unde (AI) itumike kama nyenzo ya kusaidia maamuzi ya kitaalamu, badala ya kuipa mamlaka ya kuamua mambo yanayoweza kuathiri moja kwa moja hatima ya wanafunzi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Hussein Mohamed Omar ametoa wito huo kwa wataalamu wa elimu wakati akifunga Mkutano wa 42 wa Mwaka wa Jumuiya ya Tathmini ya Elimu Afrika (AEAA) uliofanyika kwa siku nne jijini Arusha.

Dkt. Omar alisema matumizi ya AI bila kuzingatia misingi ya uadilifu yanaweza kuhatarisha usalama na uaminifu wa mifumo ya mitihani, huku yakiongeza pengo la usawa wa kielimu miongoni mwa nchi za Afrika.

"Tutumie akili bandia kuimarisha uamuzi wa kitaalamu, si kuukabidhi uamuzi huo kwa AI. Teknolojia inapaswa kusaidia wataalamu wa elimu na watahini, lakini si kuchukua nafasi yao," aliongeza Dkt. Omar.

Alisema licha ya uwezo mkubwa wa AI katika kuchakata taarifa na kusaidia shughuli za tathmini, teknolojia hiyo haiwezi kuchukua nafasi ya uamuzi wa kitaalamu katika masuala yanayohitaji uelewa wa mazingira ya mwanafunzi na jamii.

Kwa mujibu wa Dkt. Omar, AI haiwezi kuamua kwa kujitegemea iwapo swali la mtihani linaendana na utamaduni wa jamii, lina uhalali na usawa kwa wanafunzi kutoka mazingira tofauti, au limeandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya elimu.

Alisisitiza kuwa matumizi ya teknolojia katika mitihani yanapaswa kwenda sambamba na kuimarishwa kwa usalama wa mtandao, ulinzi wa taarifa, usiri wa mitihani, maadili ya kitaaluma na uwajibikaji wa taasisi.

Mkutano huo uliwakutanisha zaidi ya wajumbe 350 kutoka nchi 28 za Afrika na mabara mengine, wakiwamo maofisa wa wizara za elimu, viongozi wa mabaraza ya mitihani, wataalamu wa tathmini na wadau mbalimbali wa elimu.

Mkutano huo, uliofanyika chini ya uenyeji wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), ulijadili namna ya kuboresha mifumo ya tathmini ya elimu barani Afrika ili iendane na kasi ya maendeleo ya teknolojia, hususan matumizi ya AI. Katika mkutano huo, Tanzania kupitia Katibu Mtendaji wa NECTA, Prof. Said Mohamed, ilikabidhiwa rasmi Urais wa AEAA kwa mwaka 2026/2027 kutoka kwa mtangulizi wake, Dkt. Ashetu Gichuro kutoka Ethiopia.

Kampeni yaanzishwa Uingereza kupunguza matumizi maji wakati wa udhu

Mradi unaofadhiliwa na mdhibiti wa huduma za maji nchini Uingereza, Ofwat, umeungana na Cambridge Central Masjid kuhimiza Waislamu kupunguza matumizi ya maji wakati wa kutawadha.

Kampeni hiyo, iliyopewa jina "Reviving the Sunnah", inawahimiza waumini kutumia takribani lita moja ya maji wakati wa udhu, badala ya kuacha bomba likitiririka muda wote.

Kwa mujibu wa waandaaji, udhu wa dakika mbili chini ya bomba linalotiririka unaweza kutumia takribani lita sita za maji.

Kampeni hiyo inahusisha matumizi ya chupa zenye kipimo maalumu na ujumbe unaosisitiza kuepuka israfu, sambamba na kurejea katika mwenendo wa Mtume Muhammad (Allah amsghhushie rehema na amani) wa kutumia maji kwa kiasi.

Ofwat imesema tathmini ya mradi inaonyesha kaya zilizoshiriki zinaweza kuokoa kati ya lita 1,400 na 5,900 za maji kwa siku. Mradi huo ni sehemu ya mpango mpana wa pauni 270,000 unaolenga kupunguza matumizi ya maji katika jamii zenye tamaduni na dini mbalimbali.

Msikiti Ohio washambuliwa mara ya tatu ndani ya miaka saba

Kituo cha Kiislamu cha Westwood, Cincinnati, Ohio, kimeshambuliwa kwa mara ya tatu ndani ya miaka saba, huku viongozi wa jamii wakitaka tukio hilo litambuliwe kama uhalifu unaochochewa na chuki.

Shambulio la hivi karibuni lilitokea Agosti 3, washambuliaji wakikata waya, kuvunja dirisha na kuingia ndani ya kituo hicho kinachojumuisha msikiti na huduma za chakula kwa jamii.

Kwa mujibu wa viongozi wa kituo, wahalifu walivunja vioo vya mabango yenye aya za Qur'an, wakaiba kamera ya ulinzi na vifaa vya televisheni, huku wakiandika maneno ya matusi na neno "die" kwenye ubao.

Hakuna mtuhumiwa aliyekamatwa hadi sasa.

Viongozi wa Kiislamu wanasema tukio hilo limetokea wakati kukiwa na ongezeko la matukio na kauli za chuki dhidi ya Waislamu na Waarabu nchini Marekani.

Visa ya Umra ya mwaka mmoja yaanza Saudi Arabia

Saudi Arabia imeanzisha visa mpya ya Umra ya mwaka mmoja inayoruhusu mahujaji wa kimataifa kuingia nchini humo mara nyingi ndani ya siku 365, lakini kwa masharti ya kununua kifurushi cha huduma kwa kila safari.

Kwa mujibu wa Daily Dazzling Dawn, visa hiyo inaruhusu ukaaji wa jumla usiozidi siku 90 katika kipindi cha mwaka mmoja. Hata hivyo, kuwa na visa halali hakumwondolei msafiri wajibu wa kununua kifurushi kilichoidhinishwa kupitia mfumo rasmi wa Nusuk kila anapotaka kuingia Saudi Arabia kwa Umra.

Mahujaji pia wanatakiwa kupata kibali cha Umra kupitia programu ya Nusuk kabla ya safari.

Mfumo huo hautatumika katika kipindi maalumu cha Hajj, kuanzia mwanzo wa Dhul-Qa'dah hadi tarehe 13 Dhul-Hijjah, ambapo waumini wanaotaka kutekeleza ibada ya Hajj watahitaji vibali husika.

Hatua hiyo ni sehemu ya mpango wa Saudi Arabia kurahisisha safari za Umra huku ikidhibiti idadi ya mahujaji na huduma zinazotolewa katika maeneo matakatifu.

NA UKHTIFATIMA SS
0789 201 383

Nchi za OIC, Ulaya zalaani Israel kujitanua zaidi, hakuna hatua

Nchi za Kiislamu na mataifa kadhaa ya Ulaya zimeongeza shinikizo dhidi ya Israel kwa kulaani mpango wake wa kupanua makazi ya walowezi katika eneo la E1, Ukingo wa Magharibi, lakini hadi sasa hakuna hatua mpya ya pamoja iliyotangazwa dhidi ya Tel Aviv.

Qatar, Jordan, Umoja wa Falme za Kiarabu, Indonesia, Pakistan, Türkiye, Saudi Arabia na Misri zimetaka mpango huo usitishwe mara moja na kutoa wito wa kuchukuliwa kwa hatua za kimataifa, ikiwemo vikwazo dhidi ya watu na taasisi zinazohusika na shughuli za makazi ya walowezi.

Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Uholanzi, Canada na Norway pia zimeukataa mpango wa E1, huku Hispania ikilaani uamuzi wa Israel kutangaza zabuni za kujenga zaidi ya nyumba 1,200 katika eneo hilo.

Nchi hizo zinaonya kuwa ujenzi huo unaweza kukata mwendelezo wa kijiografia kati ya Ukingo wa Magharibi na Jerusalem Mashariki na kudhoofisha uwezekano wa kuundwa kwa taifa huru na linaloungana kijiografia la Palestina kwa msingi wa mipaka ya mwaka 1967.

Pia zimelaani vurugu zinazofanywa na baadhi ya walowezi dhidi ya Wapalestina na mali zao, na kuitaka jumuiya ya kimataifa kulinda haki ya Wapalestina ya kujitawala.

Mabalozi wastaafu wataka hatua, si maneno

Shinikizo limeongezeka baada ya wanadiplomasia wastaafu zaidi ya 100 wa Uingereza na Ufaransa kuzitaka serikali zao kwenda mbali zaidi ya matamko ya kulaani.

Katika barua ya pamoja, wametaka kusimamishwa kwa uuzaji wa silaha, biashara na makazi ya walowezi, pamoja na hatua dhidi ya kampuni zinazohusika na ujenzi wa E1.

Pia wametaka maamuzi ya mahakama za kimataifa yaheshimiwe na misaada ya kibinadamu iingie Gaza bila vikwazo.

Hata hivyo, licha ya wimbi la matamko makali na wito wa vikwazo, taarifa hizo hazijaambatana na hatua mpya ya pamoja iliyotekelezwa dhidi ya Israel.

NA UKHTIFATIMA SS
0789 201 383

Netanyahu kuita Uingereza 'Jamhuri ya Kiislamu' ishara ya mpasuko

KEJELI ya kisiasa ya Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, kuiita Uingereza "Jamhuri ya Kiislamu ya Uingereza" inaashiria mpasuko unaozidi kupanuka kati ya Serikali ya Israel na mmoja wa washirika wake muhimu, Ulaya.

Katika mahojiano na Redio ya Jeshi la Israel, Natanyahu alirejea kauli ya Makamu wa Rais wa Marekani, JD Vance, aliyewahi kutania kuwa Uingereza inaweza kuwa nchi ya kwanza "ya Kiislamu" yenye silaha za nyuklia. Serikali ya Uingereza iliita kauli hiyo "isiyokubalika kabisa."

Kiuhalisia, wote twajua Uingereza si "Jamhuri ya Kiislamu", bali ni ufalme wa kikatiba. Sensa ya 2021 ilionyesha Waislamu walikuwa 6.5% ya wakazi wa England na Wales, ingawa Pew Research Center inakadiria, idadi hiyo inaweza kufikia 17% ifikapo 2050, kutegemea kiwango cha uhamiaji.

Kwa hiyo, kauli ya Netanyahu ni ujumbe wa kisiasa kuliko uhalisia wa Uingereza.

Mpasuko kuhusu Palestina

Tofauti kati ya London na Serikali ya Netanyahu zilikuwa wazi zaidi Septemba 2025, Uingereza ilipolitambua rasmi Taifa la Palestina, ikiwa ni mabadiliko makubwa ya sera katika kulinda uwezekano wa suluhisho la mataifa mawili.

Mvutano pia umeongezeka zaidi kuhusu makazi ya walowezi. Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Uholanzi, Canada na Norway zimeukataa mpango wa Israel wa E1 katika Ukingo wa Magharibi, unaopingwa pia na nchi zote za Kiislamu na Kiarabu zilizotaka usitishwe na Israel iwajibishwe ikiwemo kuwekewa vikwazo.

E1 inapingwa kwa sababu inaweza kukata mwendelezo wa kijiografia kati ya Ukingo wa Magharibi na Jerusalem Mashariki na hivyo kudhoofisha uwezekano wa taifa la Palestina lililoungana.

Wanadiplomasia wastaafu zaidi ya 100 wa Uingereza na Ufaransa nao wamechagiza serikali zao kuchukua hatua kuhusu silaha, biashara na makazi ya walowezi.

Hivyo, kauli ya Netanyahu imekuja wakati London haijabadilisha lugha tu, bali imeanza kuchukua misimamo inayokinzana wazi na sera za waziri mkuu huyo kuhusu Palestina.

Uislamu kama hoja ya kisiasa

Kwa kuihusisha hali hiyo na Uislamu, Netanyahu anavutia washirika wapya wa mrengo wa kulia Ulaya na Marekani, akitumia hoja zao za kibaguzi kwamba ongezeko la Waislamu na wahamiaji linabadilisha utambulisho na siasa za Ulaya.

Ni hoja anayoitumia kujijenga hata katika siasa za ndani ambako anategemea washirika wa mrengo wa kulia.

Lakini Natanyahu anatuhumu kwa kidole kimoja, huku vingine vinne vikimuelekea yeye. Kwa nini ongezeko la Waislamu Ulaya liwe tishio la kisiasa na lisiwe tatizo ngezeko la walowezi wa Kizayuni maeneo ya Palestina inayokaliwa kimabavu?

Aidha, Uingereza imeeleza msimamo wake kupitia sheria za kimataifa, ushahidi wa hali ya Palestina, tishio makazi ya walowezi na makubaliano suluhisho la mataifa mawili lililokubalika kimataifa. Israel ijibu hoja kwa hoja sio kubumbabumba.

Lugha ya chuki ya Netanyahu inaweza kuongeza Uislamofobia lakini uzuri wa Uislamu unavyozidi kumulikwa kwa mibinyo na mashinikizo, haki na usahihi wake vinadhihiri. Huenda Natanyahu itasukuma watu kutaka kuujua Uislamu na kuishia kunasa zaidi kwenye uzuri wake na kuongeza ukuaji wa Uislamu.

Uingereza imeitambua Palestina, imeongeza ukosoaji wa makazi ya walowezi na kujiunga na mataifa mengine katika kuibana Serikali ya Netanyahu.

KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
0789 201383

Iwepo mikakati ya kuwavutia vijana kwenda Hijja

Mkurugenzi wa Idara ya Mashariki ya Kati katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Abdallah Kilima, amesema vijana hawapaswi kusubiri hadi wafikie umri mkubwa ndipo waanze kufikiria kutekeleza ibada ya Hijja.

Aidha, amewataka Waislamu kuachana na dhana kwamba Hijja ni ibada ya wazee pekee, akisisitiza kuwa vijana nao wanapaswa kutekeleza ibada hiyo.

Balozi Kilima alitoa kauli hiyo wakati akizungumza katika kongamano la Shirikisho la Taasisi za Hijja Tanzania Bara (TAHAFE), lililoambatana na maonesho ya taasisi zinazotoa huduma za Hijja, lililofanyika katika Ukumbi wa Lamada, jijini Dar es Salaam.

Amesema kuna umuhimu wa kuwaandaa vijana mapema kwa ajili ya ibada ya Hijja ili kujenga utamaduni wa kutekeleza ibada hiyo wakiwa na afya njema, nguvu na uwezo wa kumudu safari hiyo.

Kwa msingi huo, sisi kama Waislamu tuna wajibu wa kuweka mikakati mahsusi ya kuwahamasisha vijana kutekeleza ibada ya Hijja. Hatua ya kwanza ni kuongeza elimu kuhusu Hijja, kwa kuwa huenda baadhi ya vijana hawana uelewa wa kutosha kuhusu ibada hiyo.

Taasisi za Kiislamu, masheikh, maimamu na walinganiaji wanaweza kutumia mihadhara, darsa za misikitini, mitandao ya kijamii na programu maalumu kuwafikia vijana na kuwapa elimu kuhusu Hijja.

Vijana pia wanapaswa kuhamasishwa kuanza kuweka akiba mapema kupitia mifumo salama na inayoeleweka, badala ya kusubiri hadi watakapokuwa na fedha nyingi kwa wakati mmoja ndipo waende kuhiji.

Kwa upande mwingine, taasisi zinazotoa huduma za Hijja zina nafasi muhimu ya kuwaelimisha vijana kuhusu gharama, mipango ya malipo, maandalizi na njia salama za kuweka akiba kwa ajili ya safari hiyo.

Aidha, kuna umuhimu wa kuandaa kampeni maalumu zinazolenga vijana na kusisitiza kuwa Hijja si ibada ya wazee pekee. Kauli mbiu kama "Usisubiri Uzee, Jiandae kwa Hijja" zinaweza kutumika katika kampeni za kitaifa na mitandao ya kijamii ili kuwahamasisha vijana kuanza maandalizi mapema.

Hatua nyingine ni kuwashirikisha vijana ambao tayari wametekeleza ibada ya Hijja kutoa ushuhuda na kusimulia uzoefu wao. Ushuhuda huo unaweza kuwa na nguvu katika kuwahamasisha vijana wengine kuona kuwa Hijja ni ibada inayowezekana na inayohitaji maandalizi ya mapema.

Hatua hizo zinaweza kuwahamasisha vijana wengi zaidi kuanza maandalizi mapema, badala ya kusubiri hadi watakapokuwa na umri mkubwa, wakati ambapo nguvu na afya zao zinaweza kuwa zimepungua.



Na Said Rajab

0783 650 803

Mchango wa Uislamu katika teknolojia ya AI

SEHEMU YA 1

Teknolojia ya Artificial Intelligence (AI), inayojulikana kwa Kiswahili kama Akili Unde au Akili Mnemba na wakati mwingine huitwa Akili Bandia, mara nyingi huwasilishwa kama uvumbuzi wa kisasa uliotokana na maendeleo ya kisayansi katika ulimwengu wa Magharibi.

Chimbuko lake kama taaluma ya kisayansi lilianzia mwaka 1956, wakati mwanasayansi wa Marekani katika nyanja za Sayansi ya Kompyuta na Sayansi ya Utambuzi, John McCarthy alipotumia rasmi istilahi "Artificial Intelligence" katika mkutano wa kisayansi uliofanyika Dartmouth, Marekani.

Hata hivyo, mizizi ya dhana zinazoihusisha teknolojia hii inaenda mbali zaidi katika historia, hususan katika kipindi cha Zama za Dhahabu za Uislamu, kuanzia karne ya nane hadi karne ya 14.

Katika kipindi hicho, Wanazuoni wa Kiislamu hawakuhifadhi tu maarifa yaliyorithiwa kutoka katika ustaarabu wa Kigiriki, Kiajemi na Kihindi, bali pia waliyapanua na kuyaendeleza. Kazi zao ziliweka msingi wa dhana ambazo leo ni muhimu katika maendeleo ya AI, zikiwemo algorithms, logic, cognition na automation.

Ndugu zangu, nimeamua kuacha baadhi ya istilahi hizi za AI katika lugha yake ya Kiingereza ili kuepusha upotoshaji wa maana. Tafsiri ya istilahi hizi si suala la lugha pekee, kwani baadhi yake zina maana pana ambazo si rahisi kuwakilishwa kikamilifu kwa neno moja la Kiswahili. Hata hivyo, nitajaribu kuzifafanua kwa ufupi.



John McCarthy

Algorithm ni seti ya hatua au kanuni zinazopangwa kwa utaratibu maalumu ili kutatua tatizo, kufanya ukokotozi au kukamilisha kazi fulani.

Logic ni mfumo wa kuchunguza na kutathmini hoja ili kubaini iwapo hitimisho lake linatokana kwa usahihi na dhana au msingi uliowekwa. Dhana hii inatumika katika nyanja mbalimbali, zikiwamo falsafa, hisabati na sayansi ya kompyuta. Kwa Kiswahili, logic hujulikana kama mantiki.

Cognition ni mchakato wa kiakili unaohusisha upatikanaji wa maarifa na uelewa kupitia mawazo, uzoefu na hisia. Pia inahusisha uwezo wa ubongo kuchakata, kuhifadhi, kurejesha na kutumia taarifa katika kuendesha shughuli za kila siku. Kwa Kiswahili, huitwa utambuzi.

Automation ni matumizi ya mashine, kompyuta au programu (software) kuendesha mifumo kwa msaada mdogo wa binadamu au bila msaada wa moja kwa moja wa binadamu. Lengo lake ni kuokoa muda, kupunguza gharama, kuongeza ufanisi wa kazi na kupunguza makosa ya kibinadamu.

Makala hii inaangazia mchango wa wanasayansi wa Kiislamu katika maendeleo ya maarifa na dhana zilizokuja kuwa msingi wa teknolojia ya AI tunayoifahamu leo.

Hadithi ya Kimagharibi kuhusu chimbuko la AI

Mkutano wa Dartmouth wa mwaka 1956 unatajwa kuwa hatua muhimu katika kuanzishwa rasmi kwa AI kama uwanja wa kisayansi.

Katika mkutano huo, waanzilishi kama John McCarthy, Marvin Minsky na Claude Shannon walishiriki katika kuendeleza mijadala kuhusu uwezekano wa mashine kuiga baadhi ya uwezo wa akili ya binadamu.

Miongoni mwa dhana zilizojadiliwa ni 'computational model', yaani programu ya kompyuta au mfumo wa kihisabati unaotumika kuiga, kuchambua au kutabiri tabia ya mifumo changamano ya ulimwengu halisi.

Hata hivyo, AI kama dhana ya kutumia kanuni, mantiki na mifumo ya hatua kwa hatua katika kutatua matatizo haikuanza na kompyuta za kidijitali. Dhana kama hizo zilikuwepo karne nyingi kabla ya kuibuka kwa teknolojia ya kisasa ya kompyuta.

Muda mrefu kabla ya kuibuka kwa mashine za kisasa, Wanazuoni wa Kiislamu wa zama za kati walikuwa wameendeleza maarifa katika maeneo mbalimbali, yakiwemo matumizi ya mashine katika utatuzi wa matatizo (mechanised reasoning), mantiki ya alama (symbolic logic) na matumizi ya kanuni za hatua kwa hatua katika kutatua matatizo (algorithmic thinking).

Hizi ni baadhi ya nguzo muhimu zilizokuja kuchangia maendeleo ya AI ya kisasa. Kutambua urithi huu wa kielimu na kisayansi kunatupa uelewa mpana zaidi wa historia ya AI, kuanzia chimbuko la dhana zake, maendeleo yake hadi kufikia teknolojia tunayoiona leo.

Itaendelea wiki ijayo Insha Allah

Kosa letu kubwa ni kuishi kwa kufurahisha watu

Katika Tanzania na sehemu nyingi za Afrika, matumizi yetu hayaamuliwi na kipato pekee. Familia, marafiki, mila, mitandao ya kijamii na hamu ya kuonekana tumepiga hatua vinaweza kuwa na nguvu kubwa katika kuamua fedha zetu zinakwenda wapi.

Mtu anaweza kuongeza mshahara lakini bado asiwe na akiba. Biashara inaweza kukua, lakini mwenye biashara akaendelea kuishi kutoka mwezi mmoja hadi mwingine bila kujenga mali.

Wakati mwingine tatizo si kwamba fedha ni chache. Tatizo ni kwamba kila kipato kinapoongezeka, kiwango cha maisha nacho kinapanuka. Unapata mshahara mzuri, unaona unahitaji simu mpya. Biashara inaanza kufanya vizuri, unahisi gari ulilonalo halilingani tena na hadhi yako. Rafiki amesafiri Zanzibar au Dubai, nawe unaanza kuona safari hiyo ni lazima.

Hapo ndipo matumizi yanapoanza kuongozwa na mazingira kuliko malengo yako.

Mitandao imeongeza shinikizo

Simu janja na mitandao ya kijamii imebadilisha sana tabia za matumizi Afrika.

Leo Mtanzania anaweza kuona mgahawa mpya Instagram, mavazi TikTok, simu kupitia tangazo Facebook au bidhaa WhatsApp na kuilipia papo hapo kwa simu.

Hili limeleta urahisi mkubwa wa biashara. Lakini pia limefanya kishawishi cha kutumia fedha kiwe karibu nasi muda wote.

Tatizo ni kwamba mitandaoni tunaona zaidi kile watu walichonunua kuliko kile walichoweka akiba.

Tunaona gari, lakini hatuoni mkopo wake. Tunaona harusi nzuri, lakini hatujui familia ilitumia kiasi gani. Tunaona safari, simu na mavazi, lakini hatuoni akaunti ya benki ya mwenye navyo.

Ukilinganisha maisha yako na picha hizo, unaweza kuanza kutumia fedha kutafuta taswira badala ya kujenga maisha.

Afrika tuna nguvu ya familia — na pia shinikizo lake

Utamaduni wetu una jambo zuri sana: kusaidiana.

Tunachangia harusi, misiba, matibabu, ada, wazazi na ndugu. Huo ni mtaji mkubwa wa kijamii ambao jamii nyingi za Afrika zimeutunza kwa vizazi.

Lakini msaada unapokosa mipaka, unaweza kuharibu mipango ya kifedha. Mtu anayepata kipato anaweza kujikuta akibeba majukumu mengi kiasi kwamba hawezi kuweka akiba, kuanzisha biashara au kuwekeza.

Suluhisho si kuacha kusaidia. Ni kupanga msaada. Kama ambavyo unatenga fedha ya chakula, nyumba na usafiri, unaweza pia kutenga kiwango cha kusaidia familia na jamii. Usisubiri kila ombi liamue matumizi yako.

"Watu watasemaje?" inaweza kuwa gharama kubwa

Katika mazingira yetu, sherehe ni eneo jingine ambalo utamaduni unaweza kutawala fedha. Harusi, mahafali, sikukuu, sherehe za watoto na matukio mengine yanaweza kugeuka mashindano ya hadhi.

Mtu anaweza kutumia akiba ya miaka mingi au kuingia kwenye madeni ili kufanya tukio la siku moja lionekane kubwa. Jiulize: Ninafanya hivi kwa sababu nina uwezo, au kwa sababu sitaki watu wanione vibaya? Swali hilo linaweza kuokoa fedha nyingi.

Vijana wako kwenye shinikizo kubwa zaidi

Vijana wa Tanzania leo wanaishi katika dunia ambayo Dar es Salaam, Nairobi, Lagos, Dubai na London vinaonekana kwenye skrini moja.

Wanajifunza mitindo mipya, burudani, chakula, mavazi na teknolojia kwa kasi kubwa. Hamu ya maisha bora si tatizo. Tatizo ni kutaka kuishi leo maisha ambayo kipato chako bado hakiwezi kuyagharamia. Hapo ndipo hofu ya kubaki nyuma inapoweza kuingia.

Unanunua kwa sababu kila mtu anaonekana kununua. Unaenda mahali kwa sababu kila mtu anaonekana kwenda. Lakini kujenga utajiri kunahitaji uwezo wa kusema: "Hiki ni kizuri, lakini si lazima nikimiliki leo."

Tofautisha kuonekana tajiri na kujenga utajiri

Mtu mwenye simu ya gharama kubwa si lazima awe na fedha nyingi. Mwenye gari kubwa si lazima awe na uwekezaji. Na mtu anayeishi maisha ya kawaida si lazima awe maskini.

Utajiri halisi hujengwa kimya kimya: kwa kuweka akiba, kuwekeza, kupunguza madeni yasiyo ya lazima na kutumia chini ya kipato.

Katika Uislamu, mali ni neema lakini pia ni dhamana. Tunahimizwa kutumia vizuri bila ubakhili, lakini pia bila israfu, yaani matumizi yaliyopitiliza. Kwa hiyo kabla ya matumizi makubwa jiulize: Ningefanya hivi kama hakuna mtu ambaye angejua? Kama jibu ni hapana, huenda hununui kitu. Huenda unanunua maoni ya watu.

Mitindo itabadilika. Simu mpya itapitwa na nyingine. Gari litazeeka. Sherehe itaisha. Lakini akiba, uwekezaji na nidhamu ya fedha vinaweza kuilinda familia yako kwa miaka mingi.

Usitumie fedha kuonyesha watu umefika. Zitumie kujenga mahali unapotaka kufika.

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

ELIMU YA MAZISHI YA KIISLAMU

Nani anawajibika kuandaa mazishi ya Muislamu?

SEHEMU YA

4

Mtu anapofariki, mara nyingi husikika maneno kama: "Mwiteni Sheikh aje afanye mazishi", au "Subirini Kamati ya Msikiti ifike." Ingawa viongozi wa dini wana nafasi muhimu katika kuwaongoza Waislamu, ukweli ni kwamba Uislamu haujafanya mazishi kuwa jukumu lao peke yao. Mazishi ni wajibu wa Waislamu wote kwa ujumla.

Mazishi ni Faradhi Kifayah

Wanazuoni wamekubaliana kwamba mambi manne; kuosha maiti, kumvika sanda, kumswalia Swala ya Janaza na kumzika ni faradhi kifayah.

Maana yake ni kwamba Waislamu wakivitimiza kwa idadi ya kutosha, wengine huondokewa na dhambi, lakini ikiwa hakuna anayevifanya, jamii yote inayoweza kutekeleza wajibu huo hubeba dhambi kwa kuacha haki ya ndugu yao.

Hii inaonesha jinsi Uislamu ulivyoweka mbele mshikamano miongoni mwa Waislamu hata baada ya kifo.

Haki sita za Muislamu

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Haki ya Muislamu juu ya Muislamu mwingine ni sita..." na miongoni mwa haki hizo ni "... anapofariki, mhudhurie (janaza lake)." [Al-Bukhari na Muslim].

Kuhudhuria janaza si jambo la hiari tu la kijamii, bali ni sehemu ya haki ambazo Muislamu anastahiki kutoka kwa ndugu zake. Hata hivyo, familia ndio yenye wajibu wa kwanza kabisa.

Familia ina wajibu wa kwanza

Kwa kawaida, familia ya marehemu ndiyo yenye wajibu wa kwanza wa kuhakikisha kuwa taratibu za mazishi zinafanyika kwa mujibu wa Sharia.

Hata hivyo, ikiwa hawana elimu au uwezo wa kutosha, wanapaswa kuomba msaada kwa wale wenye ujuzi na uaminifu. Lengo si kuwapa wengine jukumu lote, bali kuhakikisha Sunna inatekelezwa kwa usahihi.

Nafasi ya Masheikh na Maimamu

Masheikh na Maimamu ni walimu wa dini wanapaswa kuwaelekeza watu, kusahihisha makosa, kuongoza Swala ya Janaza ikiwa inafaa na kuwafundisha watu namna sahihi ya kuosha na kumzika maiti.

Lakini hawa – Masheikh na Maimamu - hawapaswi kuwa watu pekee wanaojua kufanya mazishi. Ikiwa kila familia itawafundisha watoto wake namna ya kutekeleza mazishi ya Kiislamu, jamii nzima itakuwa na watu wengi wenye uwezo wa kutekeleza faradhi kifayah.

Wajibu wa jamii

Katika baadhi ya maeneo, majirani na marafiki hujitokeza mara moja kusaidia familia ya marehemu. Huu ni mwenendo mzuri uliopendekezwa na Uislamu.

Jamii – ikiwemo majirani na marafiki – wanapaswa kusaidia katika kuchimba kaburi, kuandaa sanda na kubeba maiti, ikiwemo wakati wa kwenda kuzika.

Vilevile, wasaidie kuwafariji wafiwa, kushiriki Janaza ikiwemo kusalia, ni katika matendo yanayoimarisha udugu wa Kiislamu.

Fadhila kubwa ya kushiriki janaza

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mwenye kuhudhuria Janaza mpaka akaliswalia, atapata Qirat moja. Na mwenye kubaki mpaka azikwe, atapata Qirat mbili."

Swahaba wakauliza: "Qirat mbili ni kiasi gani?" Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akasema: "Kama milima miwili mikubwa." [Al-Bukhari na Muslim].

Hii inaonesha kuwa kushiriki mazishi si kupoteza muda, bali ni ibada yenye malipo makubwa mbele ya Allah.

Makosa yanayoonekana katika jamii

Miongoni mwa makosa yanayotokea ni kudhani mazishi ni kazi ya Sheikh pekee, kusubiri mtu maalumu aje kutoka mbali ilhali watu waliopo wanaweza kutekeleza Sunna na kufanya mazishi kuwa biashara kwa kudai malipo ili kuosha au kuswalisha maiti.

Makosa mengine ni ile hali ya watu wengi kujiepusha na kushiriki Janaza wakidhani si jukumu lao na vijana kutofundishwa kabisa namna ya kuandaa mazishi.

Mkusanyiko wa haya yote husababisha jamii kupoteza elimu muhimu ambayo kila Muislamu anapaswa kuijua.

Je, tunajifunza nini?

Kila Muislamu anapaswa kujifunza angalau misingi ya mazishi ya Kiislamu. Hatufundishwi kwa sababu tutakufa leo au kesho, bali kwa sababu huenda kesho tukawa tunamhudumia mzazi wetu, mwenzi wetu, mtoto wetu au jirani yetu.

Hakuna anayejua ni lini elimu hii itahitajika kwa sababu kama tulivyoona, mazishi si jukumu la kundi maalumu la watu. Ni wajibu wa umma mzima. Kadri jamii inavyopata elimu ya mazishi ya Kiislamu, ndivyo inavyopungua utegemezi wa mila, imani potofu na desturi ambazo hazina msingi katika Qur'an na Sunna. Elimu ndiyo njia ya kuhifadhi heshima ya maiti na kutekeleza haki zake kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu.

Makala ijayo: Kuosha maiti: Hukumu, hekima na watu wanaoruhusiwa kumwosha marehemu.

DARASA
LA WIKI

SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

Haki za mke aliyepewa talaka tatu

Allah ameweka sharia ya eda kwa mwanamke aliyefiwa na mumewe, aliyepewa talaka rejea au aliyepewa talaka tatu (ba'in), kwa sababu kuu mbili.

Haki za mke aliyepewa talaka tatu

Allah ameweka sharia ya eda kwa mwanamke aliyefiwa na mumewe, aliyepewa talaka rejea au aliyepewa talaka tatu (ba'in), kwa sababu kuu mbili.

Kwanza, ni kuhakikisha hali ya kizazi chake na kuthibitisha kuwa hana ujauzito. Ikiwa ni mjamzito, eda inalenga pia kulinda ujauzito huo ili usichanganywe na mbegu ya mwanaume mwingine.

Pili, eda inalenga kuheshimu mkataba wa ndoa na utakatifu wake, pamoja na kuhifadhi athari za ndoa hiyo kwa kipindi maalumu, hata pale ambapo hakuna uwezekano wa ujauzito na kizazi cha mwanamke kiko wazi.

Kutokana na hilo, sharia imeweka kanuni zinazobainisha haki na wajibu wa mwanamke katika kipindi cha eda. Miongoni mwa masuala muhimu ni haki ya makazi. Je, mume anaruhusiwa kumtoa mwanamke aliyemtaliki katika nyumba yake?

Je, mwanamke huyo anaweza kutoka wakati wa eda ili kutimiza mahitaji na maslahi yake, au anatakiwa kubaki nyumbani katika kipindi hicho? Vilevile, je, mume anawajibika kumpa matumizi na mavazi katika kipindi cha eda, au halazimiki kufanya hivyo?

Na je, kuna tofauti kati ya mwanamke aliyepewa talaka rejea na yule aliyepewa talaka ya mwisho isiyorejea, yaani talaka tatu? Sharia zinazohusu masuala haya ziliwekwa katika hatua za mwisho za kuteremshwa kwa sheria za Kiislamu, katika mwaka wa mwisho wa uhai wa Mtume wa Allah.

Kwa sababu hiyo, hukumu hizo hazikutekelezwa mara nyingi. Hata zilipotokea, hazikuibua migogoro mikubwa kati ya wanandoa. Mume alikuwa akimridhisha mke aliyemtaliki na kumfanyia wema zaidi ya kiwango cha haki yake, huku mke na familia yake nao wakionesha moyo wa ukarimu.

Kwa sababu hiyo, mara nyingi walikuwa wakisamehe baadhi ya haki za msingi za mwanamke wakati wa talaka. Kisa cha Fatima bint Qays (Allah amridhie) na mumewe wa kabila la Makhzum ndicho kinachojulikana kuwa mgogoro uliowasilishwa kwa Mtume wa Allah.

Mtume alitoa uamuzi kuhusu suala hilo. Inawezekana hukumu hiyo ilizingatia mazingira maalumu yaliyomhusu Fatima na kwamba haikuwa sharia ya jumla inayotumika katika kila hali.

Kutokana na hilo, Wanazuoni wa Sharia ya Kiislamu wametofautiana kuhusu masuala yanayofanana na kisa chake, huku kila upande ukiwa na mtazamo wake kwa kuzingatia dalili na uelewa wa kifiqhi.

Haki ya makazi na matumizi

Wanazuoni wamekubaliana kwamba ikiwa mwanamke aliyepewa talaka tatu ni mjamzito, ana haki ya kupewa matumizi na makazi. Hata hivyo, wametofautiana kuhusu mwanamke ambaye si mjamzito. Je, anastahiki matumizi na makazi katika kipindi cha eda au hastahiki?

Katika suala hili, kuna mitazamo mitatu maarufu. Mosi, Abu Hanifa na kundi la wanazuoni wamesema kuwa mwanamke aliyepewa talaka tatu anastahiki makazi na matumizi.

Hoja yao inatokana na kauli ya Allah Mtukufu: "...Na mcheni Mwenyezi Mungu, Mola wenu. Msiwatoe (wanawake) katika nyumba zao..." [Qur'an, 65:1]. Pia kauli yake: "Wawekeni wanawake hao katika nyumba mnazoishi, kwa kadiri ya uwezo wenu." [Qur'an, 65:6].

Kwa mujibu wa mtazamo huu, aya hizo zinaelekeza mwanamke kupewa makazi katika kipindi cha eda. Kuhusu matumizi, wanazuoni hao wanaeleza kuwa mwanamke huyo amezuiliwa kuolewa na mwanaume mwingine hadi eda yake itakapokamilika.

Kwa msingi huo, wanaona kuwa haki ya matumizi inaambatana na haki ya makazi.

Pili, kuna mtazamo unaosema kuwa mwanamke aliyepewa talaka tatu hastahiki matumizi wala makazi. Hayo ndiyo maoni mashuhuri ya Imam Ahmad.

Wanazuoni wanaoshikilia mtazamo huu wanatoa hoja kwa hadith ya Fatima bint Qays (Allah amridhie), ambaye alipewa talaka tatu na mumewe. Mtume (rehema na amani zimshukie) alimwambia: "Mumeo hana wajibu wa kukupa matumizi wala makazi."

Tatu, kuna mtazamo unaosema kuwa mwanamke aliyepewa talaka tatu anastahiki makazi katika kipindi cha eda, lakini hastahiki matumizi. Haya ni maoni ya madhehebu ya Shafi'i na Malik, pamoja na kundi la wanazuoni wengi. Pia, ni moja ya riwaya mbili zilizonukuliwa kutoka kwa Imam Ahmad.

Hoja yao inatokana na dalili zilezile zilizotolewa na wanazuoni wa mtazamo wa kwanza. Wanasema aya hizo hazikutofautisha kati ya mwanamke aliyepewa talaka rejea na aliyepewa talaka isiyorejea, yaani talaka tatu. Kwa mtazamo wao, wanawake wa aina zote mbili wana haki ya kupewa makazi katika kipindi cha eda. Aidha, wameeleza kuwa muktadha wa aya unaonesha kuwa hukumu hiyo inamhusu pia mwanamke aliyepewa talaka isiyorejea.

Hata hivyo, kumpatia matumizi mwanamke aliyepewa talaka rejea ni wajibu ulio wazi katika kipindi chote cha eda yake, hata kama si mjamzito. Hii ni kwa sababu bado anahesabiwa kuwa katika ndoa ya mume wake.

Endapo mmoja kati ya mume na mke atafariki wakati wa kipindi cha eda, aliyebaki atamrithi mwenzake. Hali hiyo haitokei kwa mwanamke aliyepewa talaka tatu.

Kauli yenye nguvu

Kwa msingi huo, mtazamo unaoonekana kuwa na nguvu zaidi ni ule wa madhehebu ya Shafi'i na kundi la wanazuoni wengi, unaosema kuwa mwanamke aliyepewa talaka tatu anastahiki makazi katika kipindi cha eda, lakini hastahiki matumizi.

Afya
Pure Drinking water
"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.
WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com

MAKALA ZA WAQF

SEHEMU YA 3

NA IDARA YA ELIMU – AWQAF TANZANIA

Changamoto za kumiliki na kulinda mali za Waqf

MALI za Waqf ni miongoni mwa rasilimali muhimu zinazolenga kuhudumia jamii, kusaidia makundi yenye mahitaji na kuchochea maendeleo endelevu.

Kwa mujibu wa misingi ya Kiislamu, mali inapowekwa Waqf kwa kusudi linaloruhusiwa kisheria, inapaswa kulindwa ili manufaa yake yaendelee kunufaisha walengwa kwa vizazi. Kwa msingi huo, mali za Waqf si mali za mtu binafsi zinazoweza kutumiwa au kuhamishwa kwa matakwa binafsi.

Katika makala hii, tunajadili changamoto ya uvamizi, uporawaji wa mali za waqf na utatuzi wake kwa wakati wa sasa.

Tanzania Bara ina mali nyingi za Waqf za kihistoria — ikiwemo ardhi, viwanja, majengo ya biashara, misikiti na maeneo ya makaburi — ambazo zinakabiliwa na changamoto za kiutawala, kisheria na kiusalama.

Miongoni mwa changamoto hizo ni uvamizi wa ardhi (encroachment), migogoro ya mipaka, kupotea kwa kumbukumbu na kutokamilika kwa usajili wa kisheria.

Tatizo hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa na ukweli kwamba baadhi ya Waqf za zamani ziliwekwa kwa taratibu za wakati huo, bila kuambatanishwa na nyaraka zinazokidhi mahitaji ya mifumo ya sasa ya usimamizi wa ardhi.

Vilevile, baadhi ya wasimamizi wa awali walifariki bila kuweka mfumo mzuri wa kuendeleza usimamizi wa mali hizo. Matokeo yake, mali nyingi ambazo zilikusudiwa kuwa Waqf wa manufaa kwa jamii zimeingia katika hatari ya kupotea.

Moja ya changamoto kubwa ni uvamizi wa viwanja vya wazi na mashamba ya kihistoria.

Katika baadhi ya maeneo ya mijini na pwani, ardhi iliyowekwa Waqf miongo kadhaa iliyopita imevamiwa na kujengwa makazi, vibanda au shughuli nyingine bila idhini ya Mutawalli au taasisi inayohusika. Kukosekana kwa uzio, alama za mipaka na ulinzi wa kudumu huwarahisishia wavamizi kuanza kwa kujenga sehemu ndogo tena kidogo kidogo na hatimaye kuenea katika eneo kubwa.

Tatizo hili linaweza kuonekana pia katika baadhi ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya makaburi ya Kiislamu na shughuli za kijamii.

Eneo linapovamiwa kwa muda mrefu, jamii hujikuta ikikabiliwa na changamoto kubwa ya kutambua mipaka ya Waqf na kutenganisha matumizi halali na yale yaliyojengwa bila idhini.

Changamoto nyingine ni migogoro ya nyaraka za umiliki katika maeneo yenye thamani kubwa ya kiuchumi ambapo kwa mfano, baadhi ya majengo yaliyowekwa Waqf kwa ajili ya kusaidia mayatima, madrasa, misikiti na huduma nyingine za kijamii yalianza kwa mikataba au kumbukumbu za zamani ambazo hazijawahi kurasimishwa kikamilifu katika mifumo ya sasa ya usajili wa ardhi.

Hali hii inapokutana na mabadiliko ya mipango miji, urasimishaji au madai mapya ya umiliki, migogoro huibuka.

Maeneo kama Kariakoo na sehemu nyingine za Dar es Salaam yana historia ndefu ya mali zilizowekwa Waqf na wafanyabiashara na watu mbalimbali katika vipindi tofauti vya historia. Kwa kuwa maeneo haya yana thamani kubwa kiuchumi, mali za Waq

f zimekuwa katika hatari zaidi ya migogoro, uvamizi na mabadiliko ya matumizi.

Tatizo jingine ni kupotea kwa kumbukumbu na udhaifu wa mfumo wa uendelezaji wa usimamizi. Wakati Mutawalli au wadhamini wa zamani wanapofariki, kutokuwepo kwa kumbukumbu sahihi za Waqf, mipaka yake, masharti ya mtoa Waqf na utaratibu wa kumrithisha msimamizi huweka mali hizo katika mazingira hatarishi. Aidha, taasisi zisiposajiliwa kwa utaratibu unaotambulika kisheria, uwezo wa kuzitetea mali hizo unaweza kuwa dhaifu.

Njia tatu za kulinda mali za Waqf

Kwanza, ifanyike sensa ya kitaalamu ya mali zote za Waqf. Taasisi zinazosimamia Waqf zinapaswa kuacha kutegemea kumbukumbu za mdomo au nyaraka zilizotawanyika.

Ki msingi, kila mali iliyotolewa kama Waqf inapaswa kutambuliwa, kupimwa, kuwekewa alama za mipaka na kurekodiwa kwa kutumia teknolojia za kisasa, ikiwemo ramani za GPS na kanzi data ya kidijitali.

MAONI/ UCHAMBUZI

NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383

Ukifa, unaacha nini kama Waqf?

Zaidi ya miaka 1,400 imepita tangu Uthman bin Affan (Allah amridhie) aondoke duniani. Lakini huko Madina, historia bado inasimulia wema wake kupitia Bi-iru Rumah, kisima alichohusishwa nacho kwa kukinunua na kukifanya kiwe cha manufaa kwa watu.

Uthman hayupo. Vizazi vilivyomjua vimekwisha. Falme zimeinuka na kuanguka, mipaka imebadilika na dunia imeingia katika zama mpya. Lakini kheri aliyoianzisha bado inaendelea kuwanufaisha watu.

Hapo ndipo maana kubwa ya sadaqah jariyah inapodhihirika: mtu anaondoka duniani, lakini manufaa ya alichokitoa yanaendelea. Na kwa matumaini ya Allah, ujira wake unaendelea pia.

Ndipo swali linapokuja kwetu leo: Ukifa, utaacha nini kinachoendelea kufanya kazi baada yako katika kukuchumia thawabu endelevu?

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) amesema kwamba mtu anapokufa, matendo yake hukatika isipokuwa katika mambo matatu, miongoni mwayo ikiwa ni sadaqah jariyah—sadaka yenye manufaa yanayoendelea.

Waqf ni miongoni mwa mifumo muhimu iliyojengwa na Waislamu ili kuifanya sadaka hiyo isiwe tukio la siku moja, bali iwe manufaa yanayoendelea kwa vizazi.

Swahaba walifanya waqf kuwa utamaduni

Miongoni mwa mifano maarufu ni Umar bin al-Khattwab (Allah amridhie). Alipopata ardhi yenye thamani huko Khaybar, alimwendea Mtume (Allah amshushie rehema na amani) kumuuliza afanye nini nayo. Mtume akamshauri aihifadhi mali yenyewe na atoe manufaa yake sadaka.

Umar akaweka sharti kwamba ardhi hiyo isiuzwe, isitolewe zawadi wala kurithiwa, bali mazao yake yawafikie maskini, jamaa, wasafiri na wenye mahitaji.

Kanuni ilikuwa rahisi lakini yenye nguvu: Linda mali; tumia manufaa yake.

Uthman (Allah amridhie) alihusishwa na Bi-iru Rumah. Abu Twalha (Allah amridhie) naye alitoa bustani yake ya Bairuha, mali aliyokuwa akiipenda sana, kwa ajili ya Allah. Swahaba wengine pia walitoa mali zao kama waqf. Mwanazuoni Ibn Qudamah, katika Al-Mughni, amenukuu kutoka kwa Jabir bin Abdullah (Allah amridhie) kwamba, miongoni mwa Swahaba waliokuwa na uwezo wa mali, waqf ilikuwa jambo lililojulikana na kutekelezwa.

Hili halimaanishi kwamba kila Swahaba, tajiri au maskini, alikuwa na waqf. Lakini inaonesha kuwa kwa wale waliokuwa na uwezo, waqf haukuwa jambo la pembeni katika fikra zao kuhusu mali bali ulikuwa sehemu ya namna walivyotazama maisha na kile kitakachobaki baada ya kifo.

Waqf ulijenga ustaarabu—tulipoteza nini njiani?

Kadri Uislamu ulivyoenea, waqf haukubaki kuwa kisima, shamba au bustani. Ukawa taasisi muhimu ya kijamii.

Kwa karne nyingi, mali za waqf zilisaidia kugharamia misikiti, madrasa, taasisi za elimu, maktaba, hospitali, huduma za maji, nyumba za wasafiri na misaada kwa wenye mahitaji. Taasisi maarufu za elimu katika ulimwengu wa Kiislamu zimekuwa na historia ndefu ya kunufaika na mifumo ya waqf.

Kwa maana hiyo, waqf haukuwa tu hisani bali sehemu ya miundombinu ya jamii. Ulikuwa uwekezaji wa kijamii. Ulikuwa chombo cha kujenga ustaarabu.

Lakini katika maeneo mengi ya ulimwengu wa Kiislamu, nguvu hiyo ilianza kudhoofika. Baadhi ya mali za waqf zilipoteza thamani au zikashindwa kuendelezwa kutokana na usimamizi dhaifu, migogoro, ukosefu wa kumbukumbu sahihi na kutokuwepo kwa utaalamu wa kutosha wa kuendana na mazingira mapya ya kiuchumi.

Hali ya Tanzania

Tanzania nayo haiko nje ya changamoto hii. Zanzibar ina historia kubwa ya waqf, lakini changamoto za usimamizi, uchakavu wa baadhi ya mali, migogoro na hitaji la kuongeza utaalamu, uwazi na uwezo wa kuzalisha mapato zinahitaji kupewa uzito unaostahili.

Hili linapaswa kutushtua kwa sababu mahitaji ya jamii hayajapungua bali yanaongezeka.

Tuna watoto wanaohitaji elimu, vijana wanaohitaji mafunzo na fursa za kiuchumi, familia zenye mahitaji, wagonjwa wanaohitaji matibabu, wanafunzi wanaohitaji ufadhili, pamoja na jamii zinazohitaji maji, makazi na huduma nyingine muhimu.

Lakini mara nyingi jibu letu limekuwa lilelile: tunakusanya mchango leo, kesho tunakusanya tena, na wiki ijayo tunarudia.

Sadaka ya kawaida ni muhimu sana. Inasaidia kukabiliana na mahitaji ya haraka na inaweza kuokoa maisha. Lakini kwa baadhi ya mahitaji ya kudumu, tunahitaji pia mfumo unaoweza kuzalisha manufaa kwa muda mrefu.

Hapo ndipo waqf unapokuja na fikra tofauti: Badala ya kutumia kila kitu leo, tunajenga kitu kitakachozalisha manufaa kesho.

Waqf wa kizazi chetu unaweza kuwa nini?

Fikiria jengo la maduka ambalo kodi yake inalipia ada za watoto wenye mahitaji kila mwaka, shamba ambalo mapato yake yanaendesha madrasa, nyumba ambayo kodi yake inasaidia matibabu ya wagonjwa wasiojiweza.

Si hayo tu, kwa ukubwa zaidi, fikiria mfuko wa fedha ambao mapato yake halali yanatoa ufadhili wa masomo kila mwaka. Huo ndio uwezo wa waqf.

Na leo si lazima uwe na ardhi kubwa kama Umar (Allah amridhie), wala kisima kama Bi-iru Ru mah. Waqf inaweza kuwa shamba, kiwanja, nyumba, duka, jengo la biashara au sehemu ya mali inayowekwa kwa kusudi la waqf.

Waqf wa fedha

Katika mazingira ya sasa, pia kuna mjadala na matumizi ya cash waqf (waqf wa fedha), ambapo fedha huwekwa na kuendeshwa au kuwekezwa kwa njia inayokubalika kisharia, huku manufaa yake yakielekezwa kwenye kusudi lililowekwa.

Hili linaweza kupanua ushiriki wa watu wengi zaidi. Mtu asiye na nyumba, shamba au kiwanja anaweza kushiriki kwa uwezo wake, na watu wengi wanaweza kuunganisha michango yao kujenga mfuko mkubwa wa waqf.

Hata hivyo, waqf wa kisasa unahitaji zaidi ya nia njema. Unahitaji usimamizi mzuri ili kuwe na ufanisi na malengo yafikiwe. Hili linatuleta kwenye jambo la utawala bora.

Unahitaji utawala bora

Mali zisajiliwe. Hati zilindwe. Hesabu zikaguliwe. Mapato yajulikane. Wadau waelezwe mali ya Allah iliyowekwa kwa ajili yao inafanya nini. Wasimamizi wawe waaminifu na wenye uwezo. Mali ziendelezwe kitaalamu na, inapowezekana, zizalishe mapato yanayoongeza manufaa yake.

Haya ni muhimu sana kwa sababu waqf usiosimamiwa vizuri unaweza kubaki jengo lililofungwa, shamba lisilolimwa au kiwanja kinachogombaniwa kwa miaka mingi.

Waqf wa karne ya 21 hauwezi kutegemea kumbukumbu zilizoko kichwani mwa mtu mmoja na daftari lililochakaa. Waqf wa zama hizi unahitaji mfumo, uwazi, maarifa, uwekezaji na zaidi ya yote, unahitaji uaminifu.

Utaacha nini baada yako?

Nukta ya muhimu zaidi ni tukumbushane kuwa siku moja tutakuwa marehemu. Nyumba tutaziacha. Akaunti tutaziacha. Viwanja tutaviacha. Biashara tutaziacha. Mali zetu zitagawanywa kwa mujibu wa taratibu zinazostahili.

Jina letu litabaki katika kumbukumbu za wanaotupenda — na polepole, hata kumbukumbu hizo zitafifia. Lakini tunaweza kuacha kitu kingine kitakachodumu na kutunufaisha huko Akhera.

Kitu kinachomfundisha mtoto ambaye hatujawahi kukutana naye. Kinachompa maji mtu ambaye hajawahi kusikia jina letu. Kinachomsaidia mgonjwa ambaye hatujawahi kumuona. Kinachomlipia mwanafunzi ada miaka 30 baada ya sisi kuondoka.

Huo ndio urithi wa waqf, utaratibu aliotuachia Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

Uthman bin Affan (Allah amridhie) aliondoka duniani zaidi ya karne 14 zilizopita. Lakini kisa cha Bi-iru Rumah bado kinatukumbusha kwamba mali inaweza kuondoka mikononi mwa mwenye nayo, lakini manufaa yake yanaweza kuendelea kuishi.

Swali si tu kwamba utawaachia warithi wako nini. Swali kubwa zaidi ni Ukifa, umeacha nini kama waqf?

ربيع أول

فتاوى

Kujilipisha faini kwa kuchelewa kulipa mkopo kikundini ni riba?

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Swali: Kwenye moja ya vikundi vya kukopeshana bila riba, mwanakikundi mmoja amenukuliwa akisema: "Kwa kuwa nimechelewa kulipa deni langu kwenye kikundi, basi nitalipa na faini." Swali langu, je, kuulipa huo mkopo na faini, ambayo mtu amejiwekea yeye mwenyewe, ni riba?

Jawabu: Ndiyo, ikiwa faini hiyo imewekwa kwa sababu ya kuchelewa kulipa mkopo, kwa hukumu ya Sharia hiyo ni riba, hata kama mkopaji mwenyewe ndiye aliyesema kwa hiari: "Kwa kuwa nimechelewa, nitalipa na ziada."

Sababu ni kwamba kinachozingatiwa si nani aliyependekeza malipo ya ziada, bali ziada hiyo imefungamanishwa na deni kwa sababu ya muda/ucheleweshaji.

Kwa mfano, Mwana kikundi alikopa TSh 100,000 na alipaswa kurejesha TSh 100,000. Lakini alipochelewa, akasema: "Kwa kuwa nimechelewa, nitalipa TSh 110,000." Hiyo TSh 10,000 ya ziada ni riba ya deni, kwa sababu imeongezeka kutokana na kuchelewa kwa malipo.

Itabaki kuwa ni riba hata kama hakulazimishwa ni yeye mwenyewe aliyejitolea, hata kama kikundi hakikuomba bali alikusudia kuonesha uwajibikaji. Hayo yote hayabadili hukumu ya ziada hiyo ikiwa sababu yake ni kuchelewa kulipa deni.

Lakini kuna tofauti muhimu ya kuzingatia.

Ikiwa mtu amelipa deni lake lote kwa wakati, kisha akaamua kwa hiari yake kutoa kiasi cha ziada kama zawadi, bila makubaliano ya awali wala sharti lolote, hiyo inaweza kuwa zawadi (hiba) na si lazima iwe riba. Kwa mfano, amekopa TSh 100,000, akarudisha TSh 100,000 kwa wakati, halafu akasema, "Nimefurahia huduma ya kikundi, chukueni TSh 5,000 kama zawadi" kwa vyovyote hiyo ni tofauti na kusema: "Nimechelewa, kwa hiyo nitaongeza TSh 5,000."

Nasaha kwa kikundi

Kama lengo la kikundi ni kukopeshana kwa msingi wa Qardhwan Hasan (mkopo mwema bila riba), ni vizuri kuweka kanuni kwamba mkopaji haruhusiwi kuongeza kiasi chochote juu ya deni kwa sababu ya kuchelewa kwake.

Lakini kama mnataka kuweka utaratibu wa kuwawajibisha wanaochelewesha malipo, au namna ya kumshughulikia mwanakikundi anayekataa au kuchelewesha kulipa bila udhuru, kuna njia nyingine zinazoweza kuchunguzwa kisheria bila kuifanya ziada hiyo kuwa faida ya mkopeshaji. Kwa mfano, katika baadhi ya mifumo ya Sharia, suala la faini ya mkiukaji wa makusudi (gharamah) lina masharti maalumu na haiwezi kuchukuliwa tu kuwa ni "riba ya kuchelewa." Kwa hiyo, msichukulie faini ya kuchelewa kama jambo la kawaida la kuongeza kwenye mkopo.

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Swali: Kuna taratibu zozote zinazoweza kuwekwa na kikundi cha kukopeshana ili kuepuka riba?

Jawabu: Ndiyo. Kwa kikundi cha kukopeshana bila riba (Qardhwa Hasan), mnaweza kuweka utaratibu wa kushughulikia ucheleweshaji bila kugeuza deni kuwa chanzo cha faida.

Kwanza, mumtenganishe mwenye udhuru na mwenye uwezo anayekataa. Qur'an imeweka wazi: "Na ikiwa mwenye deni yuko katika hali ya dhiki, basi apewe muda mpaka awe na uwezo." [Qur'an, 2:280].

Kwa hiyo, kama mwanakikundi hana uwezo wa kulipa kwa ukweli, asiadhibiwe kwa faini bali apewe muda au mpango mpya wa malipo.

Lakini kama ana uwezo wa kulipa halafu anakusudia kuchelewesha bila sababu, huo ni uzembe na dhulma. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Kuchelewesha kwa mwenye uwezo ni dhulma." [Bukhari na Muslim].

Pili, muweke mwanakikundi mwenye uwezo chini ya utaratibu wa uwajibikaji. Badala ya kusema: "Umechelewa, kwa hiyo deni lako limeongezeka", semeni: "Deni lako linabaki kuwa lilelile, lakini umevunja masharti ya uanakikundi kwa kuchelewesha bila udhuru."

Hapo mnaweza kuwa na hatua kama kukumbushwa na kupewa muda mfupi wa kurekebisha hali, kuitwa na uongozi wa kikundi ili kueleza sababu ya kuchelewa na kusimamishwa kupata mkopo mwingine mpaka amalize deni lake.

Hatua nyingine, ikiwa ni tabia ya kurudia, anaweza kusimamishwa au kuondolewa kwenye mfumo wa mikopo wa kikundi, kwa mujibu wa kanuni zenu.

Ikiwa kuna ushahidi wa uwezo na kukataa kabisa kulipa, kikundi kinaweza kuchukua hatua za kisheria za kudai haki yake, bila kuongeza riba kwenye deni.

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

MAKALA MAALUM

Na Said Rajab
0783 650 803

Ahadi ya Mus'ab bin Umayr kwa Allah



SEHEMU YA MWISHO 3

Katika makala iliyopita tulishia na aya isemayo: "Na hakuwa Muhammad ila ni Mtume tu. Wamepita kabla yake Mitume. Je, akifa au akiuwawa ndiyo mtageuka nyuma mrudi mlikotoka (kwenye ukafiri)? Na atakayegeuka nyuma akarudi alikotoka, huyo hatomdhuru chochote Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu atawalipa wenye kushukuru." [Qur'an, 3:144].

Aya hiyo ilifunuliwa kwa Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie), ikiakisi maneno ya Mus'ab bin Umayr (Allah amridhie) katika vita vya Uhud vilivyopiganwa jirani na mlima Uhud mnamo mwaka 625 AD kati ya Maswahaba wa Madina (Answar) na jeshi la Makureish wa Makka.

Katika siku hiyo ya vita, Mus'ab alipoteza mikono yake yote miwili kutokana na mashambulizi ya adui. Akiwa bado ameishikilia bendera kwa kutumia mabaki ya mikono yake alichomwa mkuki. Alipoanguka, alijifariji kwa kukumbuka kwamba: "Muhammad ni Mtume tu."

Kwa kuzingatia hayo yote, tunapomkumbuka Mus'ab (Allah amridhie) tunahitaji kutambua kwamba ingawa alimpenda sana Mtume, lakini mapambano yake yalikuwa kwa ajili ya Allah Mtukufu.

Tangu aliposilimu, Mus'ab alielewa vyema kwamba ahadi yake ilikuwa kwa Allah 'Azza wa Jallah. Kwa hiyo, aliamua kutumia juhudi zake zote kutimiza ahadi hiyo kwa Allah, akionesha kwamba misiba na hasara havipaswi kuwa sababu ya kujiondoa katika majukumu yetu kama Waislamu.

Badala yake, alitaka kuonesha kwamba hali hizo ni kichocheo zaidi cha kuthibitisha uaminifu na upendo wetu kwa Allah ili tutegemee rehema zake Siku ya Kiyama.

Leo hii, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) hayupo tena duniani, lakini tumebaki na Qur'an na Sunna zake kama mwongozo wa maisha yetu. Hata hivyo, bado tunakabiliwa na changamoto na mashambulizi kutoka pande mbalimbali duniani.

Jitihada za kusimamisha Uislamu zimegeuzwa kuwa uhalifu mkubwa badala ya rehema! Tunahitaji kutafakari – je, tutapoteza mwelekeo wetu wakati wa mgogoro huu, au tutainua bendera ya Uislamu juu na kuendeleza misheni ya Mtume?

Je, tutajifariji kwa maneno ya Qur'an na ahadi za Allah 'Azza wa Jallah' kama alivyofanya Mus'ab (Allah amridhie) au tutakuwa miongoni mwa walioshindwa?

Mus'ab (Allah amridhie) hakushuhudia dola ya kwanza ya Kiislamu iliyoanzishwa na Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie), lakini kwa idhini ya Allah atapata daraja ya juu ya Pepo.

Hebu tupitie upya nia zetu kwa kutafakari aya ambayo Mtume aliisoma alipoiona maiti ya Mus'ab, aliyeuawa shahidi katika eneo la Uhud: "Miongoni mwa Waumini wapo watu waliotimiza waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwishakufa (mashahidi), na baadhi wanangojea (zamu yao), wala hawakubadilisha ahadi yao hata kidogo." [Qur'an, 33:23].

ربيع أوّل

DARASA LA WIKI

SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

Adabu za kuzingatia unapoalikwa kwenye walima

SEHEMU YA 1

Katika makala iliyopita, tulibainisha sharia mbalimbali zinazohusiana na mwaliko wa dhifa ya chakula cha harusi (walima). Tulisema kuwa kuitikia mwaliko wa dhifa ya walima ni wajibu kwa mujibu wa maandiko mbalimbali. Hata hivyo, ikiwa sharti mojawapo halitatimia, kuhudhuria dhifa hiyo hakutakuwa wajibu. Katika makala hii ya pili na ya mwisho, tutataja masharti yanayopaswa kutimia katika walima ili aliyealikwa awe na wajibu wa kuhudhuria.

Mosi, aliyealikwa ahusishwe yeye binafsi na mwaliko huo

Mwalikaji anapaswa kumhusisha aliyealikwa kwenye walima – ima kwa kumwalika yeye binafsi kupitia mwakilishi wake au kwa njia nyingine inayoonesha wazi kwamba mwaliko huo umemlenga yeye binafsi.

Katika hali hiyo, ni lazima kuitikia mwaliko huo. Hata hivyo, ikiwa mwaliko ni wa jumla na haumlengi mtu au kundi maalumu, si lazima kuuitikia. Kwa hiyo, mtu ambaye hakulengwa binafsi katika mwaliko huo halazimiki kuitikia, wala hatapata dhambi kwa kutohudhuria.

Pili, mwaliko usitanguliwe na mwaliko mwingine

Mtu akialikwa na watu wawili, ikiwa anaweza kuhudhuria mialiko yote miwili ni lazima aitikie yote ikiwa muda unaruhusu. Lakini ikiwa hawezi kuikusanya mialiko yote miwili, basi ni lazima aitikie mwaliko wa yule aliyemtangulia kumwalika.

Tatu, kuepuka maovu

Wakati wa kula chakula cha walima, haipaswi kuwepo jambo lolote ovu lililokatazwa, kama vile pombe, nyimbo zilizoharamishwa zinazohamasisha zinaa, ulevi na matusi, pamoja na vyombo vya muziki.

Mtume (rehema na amani za Allah zimshukie) amesema: "Atakayeona jambo ovu miongoni mwenu aliondoe kwa mkono wake. Asipoweza, basi aliondoe kwa ulimi wake (yaani alikemee); na akishindwa, basi alichukie moyoni mwake. Na huo ni udhaifu wa imani." [Muslim].

Adabu za walima

Kuna adabu mbalimbali za walima ambazo Muislamu anapaswa kuzizingatia ili kuhakikisha kuwa dhifa hiyo inafanywa kwa kuzingatia misingi ya sharia.

Mosi, dhifa ifanywe kwa ikhlas

Muislamu hapaswi kuandaa dhifa ya walima kwa kutumia mali nyingi kwa lengo la kupata sifa na pongezi kutoka kwa watu. Badala yake, anapaswa kufanya hivyo kwa ikhlas na kwa kutafuta radhi za Allah.

Kwa masikitiko makubwa, tamaa ya sifa na kujionyesha (ria) imekuwa miongoni mwa sababu zinazowafanya baadhi ya watu kutumia gharama kubwa kujifaharisha na kushindana katika kuandaa walima.

Pili, kuwajumuisha masikini

Dhifa ya chakula cha walima inapaswa kuwaunganisha jamaa, majirani na watu wanaofahamiana, bila kujali hali zao za kifedha. Kuwaalika matajiri pekee na kuwapuuza masikini ni jambo ovu lililo wazi.

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Chakula kibaya zaidi ni chakula cha walima (harusi), ambacho matajiri hualikwa (ilhali hawakihitaji) na masikini huachwa." [Sahih Bukhari].

Tatu, kuepuka ubadhirifu

Baadhi ya watu, kwa mfano, huwaalika wageni 10 lakini huandaa chakula kinachoweza kuwatosha watu 30. Mwishowe, chakula kinachobaki hutupwa kwenye mapipa ya taka au maeneo ya kutupia uchafu. Huu ni miongoni mwa ubadhirifu uliokatazwa.

Allah Mtukufu anasema: "Na kuleni na kunyweni, wala msifanye ubadhirifu. Hakika Yeye (Allah) hawapendi wafanyao ubadhirifu." [Qur'an, 7:31]. Pia, baadhi ya watu hufanya ubadhirifu kwa kukodisha kumbi za harusi kwa gharama kubwa, licha ya kutokuwa na uwezo wa kugharamia shughuli hiyo.

Mara nyingi hufanya hivyo kwa lengo la kujionyesha na kujifaharisha. Hali hiyo pia hujitokeza katika suala la mahari na vifaa vinavyoandaliwa kwa ajili ya bibi harusi.

Jambo bora ni kuzingatia kiasi na kuwa na matumizi ya wastani. Imesimuliwa kuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) hakuwahi kupewa hiyari kati ya mambo mawili isipokuwa alichagua lililo jepesi zaidi, maadamu halikuwa jambo la dhambi. [Bukhari].

Mtume alipomuoa Zainab (Allah amridhie) aliandaa walima. Hiyo ilikuwa miongoni mwa dhifa kubwa alizowaandalia wake zake. Alichinja kondoo mmoja, akagawa nyama yake, na watu wengi wakala chakula hicho.

Nne, kuepuka maasi na mambo ya ovyo

Miongoni mwa mambo yanayofanyika katika baadhi ya dhifa za walima ni wanawake kuhudhuria wakiwa wamejipamba kupita kiasi, kana kwamba wao ndio wanaosindikizwa kwenda kwa waume zao. Inashangaza kuona mwanamke akijipamba kwa kiwango kikubwa katika dhifa ya walima ilhali mapambo hayo hayatumii akiwa nyumbani kwake. Aidha, baadhi ya watu hutumia fursa ya dhifa za walima kuwatambulisha mabibi harusi kwa wanaume wengine huku wakiwa wamejipamba. Vilevile, wapo mabibi harusi wanaowatambulisha waume zao mbele ya wanawake waliojipamba.

Hali hii ni ishara ya kushangaza ya kukosekana kwa wivu. Unaweza kujiuliza: Je, mwanamke huyo ameolewa na mwanaume mmoja au wanaume wengi? Jambo hili halikubaliki katika mila zetu wala katika sharia yetu.

Kabla hujafa, hakikisha unachoacha mtandaoni kina kheri

Mitandao ya kijamii imekuwa kiungo muhimu katika maisha yetu ya kila siku. Kupitia mitandao hiyo, tunashiriki sehemu kubwa ya maisha yetu kwa njia ya ujumbe mfupi wa maneno, picha, video, sauti, nyaraka, maoni, machapisho na kumbukumbu mbalimbali.

Leo hii, unaweza kufikia mitandao ya kijamii popote ulipo kwa kutumia simu au kompyuta. Lakini siku utakapofariki na kuzikwa, utaacha kila kitu nyuma. Simu haitakwenda kaburini pamoja nawe, wala mitandao ya kijamii haitakuwa sehemu ya sanda yako.

Hata hivyo, unachoweka mtandaoni kinaweza kuendelea kuwepo na kuacha athari kwa muda mrefu baada ya wewe kuondoka duniani. Qur'an inabainisha kuwa matendo ya mwanadamu hayaishii pale anapoyafanya. Allah Mtukufu anasema: "Hakika Sisi tunawahuisha wafu, na tunaandika waliyoyatanguliza na athari zao." [Qur'an 36:12].

Aya hii inatukumbusha ukweli muhimu kuhusu maisha ya mwanadamu: kila tunachofanya duniani huacha alama nyuma yetu. Katika zama hizi za mitandao ya kijamii, athari tunazoacha nyuma zinaweza kuwa kubwa zaidi kuliko tunavyodhani.

Maudhui tunayochapisha yanaweza kusambaa kwa kasi, kuwafikia maelfu ya watu na kubaki mtandaoni kwa miaka mingi. Leo hii, mtu anaweza kupokea video yenye maudhui machafu na kuisambaza kwa marafiki zake akidhani kuwa ni jambo la kawaida au la kujifurahisha.

Hata hivyo, kinachoonekana kama mzaha wa muda mfupi kinaweza kugeuka kuwa chanzo cha madhara makubwa, kuwaathiri wengine na kuendelea kusambaa mitandaoni kwa muda mrefu.

Ni muhimu kutambua kuwa mitandao ya kijamii si jukwaa la burudani pekee. Kila maudhui yanayowekwa mtandaoni yanaweza kuwa na athari kwa wengine na hivyo kuwa sababu ya mtu kuandikiwa madhambi au thawabu, kutegemea aina ya maudhui anayoshiriki na matokeo yake.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mwenye kulingania katika uongofu atapata ujira sawa na wale wanaomfuata, bila kupunguza chochote katika ujira wao; na anayelingania upotevu atapata madhambi sawa na wale wanaomfuata, bila kupunguza chochote katika madhambi yao." [Sahih Muslim, hadith namba 2674].

Hivyo, kila neno, picha, video au ujumbe unaoweka mtandaoni unaweza kuwa sehemu ya athari utakayoiacha duniani – iwe ya kheri au ya shari. Unachochapisha leo kinaweza kuendelea kusambaa na kuwafikia wengine, hata baada ya muda mrefu.

Ndiyo maana, kabla ya kubonyeza "Post", "Send" au "Share", ni muhimu kutafakari kwa makini: Je, ninachotuma ni cha kweli? Kina manufaa? Kinaweza kumdhuru mtu? Au kinaweza kuniletea dhambi badala ya thawabu?

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Anapofariki mwanadamu, matendo yake yote hukatika isipokuwa mambo matatu: sadaka yenye kuendelea, elimu yenye manufaa, au mtoto mwema anayemuombea dua." [Muslim na wengineo].

Kwa msingi huo, kabla ya kuchapisha chochote mtandaoni, ni muhimu kutafakari thamani na athari ya kile unachowaachia wengine. Jiulize: Je, nimeacha maarifa sahihi au ujumbe unaowaelekeza watu kwa Allah? Je, video, sauti au maneno niliyowahi kutuma yatakuwa sababu ya wengine kufanya mema au mabaya?

Haya ni maswali muhimu na ya msingi kwa sababu, Siku ya Kiyama utawajibika kwa yale unayoyasikia, unayoyaona na unayoyafuata. Hata kile unachokichapisha na kuwaachia wengine kinaweza kuwa sehemu ya hesabu yako.

Kwa hiyo, matumizi ya mitandao ya kijamii hayawezi kutenganishwa na uwajibikaji wa kidini. Ndugu yangu Muislamu, kila unapokagua akaunti zako za mitandao ya kijamii, chukua fursa pia kujitathmini.



Jiulize ikiwa maudhui unayochapisha, kushiriki au kuyapenda yanaendana na maadili na misingi ya Uislamu.

Zaidi ya hayo, jiulize swali hili kwa uaminifu: "Ikiwa nitakufa leo, ningependa maudhui haya yaendelee kuwepo?" Kama jibu ni hapana, usisubiri. Futa yale yanayopaswa kufutwa, acha yanayofaa kubaki, kisha tubia kwa Allah.

Ikiwa kuna jambo jema unaloweza kufanya kupitia mitandao ya kijamii, lifanye leo, kwani athari za maudhui utakayoacha zinaweza kuendelea kuwafikia, kuwagusa na kuwanufaisha watu kwa miaka mingi ijayo na kukupatia thawabu hata baada ya kufa.

ربيع أول

NA ZAHARANI BARAKA

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

Hivi ndivyo Swahaba walivyompenda Mtume

Urwah bin Mas'ud (Allah amridhie) alikuwa miongoni mwa wajumbe wa Makureish waliomtembelea Mtume (rehema na amani zimshukie) wakati wa mazungumzo ya suluhu ya Hudaibiya.
Aliporejea kwa watu wake, alieleza kwa mshangao mkubwa namna Maswahaba walivyomheshimu na kumpenda Mtume. Akasema: "Enyi watu! Wallahi, nimewafikia wafalme; nimefika kwa Kaisari, Kisra na Najashi. Wallahi, sijawahi kumuona mfalme yeyote anayeheshimiwa na watu wake kama Muhammad anavyoheshimiwa na Maswahaba wake." *[Bukhari]*.

Kauli hizi za Urwah zinaonesha wazi kiwango kikubwa cha upendo na heshima ambacho Maswahaba walikuwa nacho kwa Mtume (rehema na amani zimshukie). Urwah alishuhudia mwenyewe kwamba kila Mtume alipotoa amri, Maswahaba waliharakisha kuitekeleza.

Wakati wa kutawadha, walishindana kupata maji yaliyobaki baada ya udhu wake. Alipokuwa akizungumza, walimsikiliza kwa utulivu na heshima kubwa bila kumkodolea macho kwa sababu ya kumheshimu.

Upendo wao haukuwa wa maneno pekee, bali uliambatana na utiifu, kujitolea, kumlinda, kufuata Sunna zake na kuvumilia kila aina ya maudhi kwa ajili ya dini aliyokuja nayo.

Kwao, kumpenda Mtume kulimaanisha pia kufuata mafundisho yake na kusimama pamoja naye katika kila hali. Hivyo, upendo wao ulionekana wazi kupitia matendo yao ya kila siku.

Miongoni mwa waliodhihirisha upendo huo kwa dhati alikuwa Umar bin Khattwab

(Allah amridhie). Mtume (rehema na amani zimshukie) alimweleza Umar kuwa imani ya mtu haitakamilika mpaka Mtume awe kipenzi kwake kuliko nafsi yake.

Umar akasema: "Sasa, Wallahi wewe ni kipenzi kwangu kuliko nafsi yangu." Mtume akamwambia: "Hivi sasa, ewe Umar umekuwa Muumini wa kweli)." Katika vita vya Uhud, Maswahaba wengi (Allah awaridhie) walijitahidi kwa nguvu zao zote kumlinda Mtume dhidi ya maadui.

Miongoni mwa Maswahaba hao alikuwa Twalhah bin Ubaydillah, ambaye alijitolea kwa dhati kumlinda Mtume (rehema na amani zimshukie) hadi mkono wake ukapata majeraha makubwa.

Tukio hili linatupa nafasi ya kujiuliza: Tunapodai kumpenda Mtume, je, tunafuata Sunna yake na kushikamana na mafundisho aliyotuachia? Je, tunapenda yale aliyoyapenda na kuyaacha yale aliyoyakataza?

Au tunabuni njia na taratibu nyingine zinazopingana na mwenendo wake, kisha tunazifanya kuwa alama ya upendo wetu kwake?

Mapenzi ya uongo

Tumeingia mwezi wa Rabiul–Awwal, unaojulikana pia kama Mfungo Sita, ambapo katika maeneo mbalimbali hujitokeza mijadala na shughuli zinazohusishwa na madai ya kumpenda Mtume. Hata hivyo, upendo wa kweli haupaswi kupimwa kwa wingi wa sherehe, mikusanyiko au mashairi, bali kwa kiwango cha mtu kufuata mafundisho ya Mtume.

Katika kipindi hiki, mialiko ya maulidi huonekana katika maeneo mbalimbali, huku baadhi yake ikiambatana na nyimbo, dufu na ala za muziki. Jambo la msingi kwa Muislamu ni kujiuliza iwapo namna hiyo ya kuonesha mapenzi inaendana na mwenendo wa Mtume na Maswahaba zake.

Maswahaba walizingatia kwa dhati maelekezo ya Mtume kuhusu kushikamana na Qur'an na Sunna. Walipinga na kukemea mwenendo wowote unaokwenda kinyume na mafundisho hayo, hata pale ambapo aliyefanya jambo hilo alikuwa na nia njema ya kujikurubisha kwa Allah.

Kwa hiyo, nia njema pekee haitoshi ikiwa njia inayotumika haikubaliki katika mafundisho ya dini. Upendo wa kweli unahitaji kufuata njia aliyoiacha Mtume.

Tuwe Ahlus Sunnah wa kweli

Ahlus Sunnah Wal–Jamaa'ah ni wale wanaoshikamana na Qur'an na Sunna kwa uelewa wa wema waliotangulia. Wameifanya Qur'an na Sunna kuwa msingi wa maneno na matendo yao, wakatosheka navyo na kuwaalika watu kuvifuata kwa elimu, hekima na ikhlas.

Wao hushikamana na kamba ya Allah, uongofu wa Mtume wake na mwenendo wa wema waliotangulia. Katika masuala mbalimbali ya Sunna, hushikamana na njia ya kati; hawapindukii katika dini wala hawazembei.

Al–Hafidh Ibn Rajab (Allah amrehemu) amesema kwamba Sunna kamili ni njia iliyo salama kutokana na shubha na matamanio. Kauli kama hiyo pia imenukuliwa kutoka kwa baadhi ya wanazuoni waliotangulia, akiwamo Hasan al–Basri, Yunus bin Ubayd, Sufyan na Al–Fudhayl.

Tuzipe nafasi Sunna zilizosahaulika

NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383

Uwezo tunao, tunachokosa ni uratibu wa umma

Katika michezo kuna msemo unaojirudia mara nyingi: timu fulani ina wachezaji wazuri, lakini haina timu.

Maana yake ni rahisi. Unaweza kuwa na watu wengi wenye vipaji, lakini kama hakuna uratibu unaowaunganisha, vipaji hivyo haviwezi kutoa matokeo yanayotarajiwa.

Katika mchezo wa kuvuta kamba, kwa mfano, ushindi hautokani tu na kuwa na watu wenye nguvu. Siri kubwa ni kuvuta pamoja, kwa wakati mmoja na kuelekea upande mmoja. Watu wanane wenye nguvu wanaovuta kila mmoja kwa wakati wake wanaweza kushindwa na watu wenye nguvu za kawaida wanaovuta kwa mpangilio.

Soka nalo linatufundisha jambo hilo. Huwezi kuweka wachezaji 11 uwanjani halafu ukawaambia kila mmoja aonyeshe kipaji chake. Lazima mmoja awe golini, wengine walinde, wengine wajenge mashambulizi na wengine wafunge mabao. Zaidi ya hapo, lazima kuwe na mfumo unaowaunganisha.

Natumia mifano hiyo kuelezea jambo ambalo naamini Umma wa Kiislamu nchini Tanzania unahitaji kulitafakari kwa kina.

Tuna watu, lakini tunawatumiaje?

Mara nyingi ninapoingia misikitini na kuangalia safu za waumini, huwa najiuliza: tunajua kweli hazina iliyopo humu?

Katika safu moja unaweza kukuta daktari, mwalimu, mhandisi, mwanasheria, mhasibu, mfanyabiashara, mkulima, mwanahabari, fundi, kijana mwenye maarifa ya teknolojia na mtu mwenye mtandao mkubwa wa kijamii.

Wote wanaswali pamoja.

Lakini baada ya swala kila mmoja anaondoka na kipaji chake. Swali ni: uwezo huo wote unakusanywaje kwa ajili ya kuijenga jamii?

Hatuwezi kusema hatuna watu. Tunao.

Hatuwezi kusema hatuna utaalamu. Tunao.

Hatuwezi kusema hatuna wafanyabiashara, wasomi au vijana wenye uwezo. Wapo.

Changamoto yetu kubwa inaweza kuwa kutokuwa na mifumo inayowatambua, kuwaunganisha na kuwaelekeza katika malengo makubwa ya pamoja.

Wengine wameweza, kwa nini sisi tushindwe?

Duniani tunaona jumuiya mbalimbali zikijenga shule, hospitali, vyuo, vituo vya kulea watoto, taasisi za misaada, mashirika ya habari na miradi mikubwa ya kijamii.

Mambo hayo hayafanyiki kwa sababu watu wao wote ni matajiri.

Yanafanyika kwa sababu kuna uongozi unaokusanya vipaji, fedha, maarifa na muda wa watu na kuvipeleka katika lengo moja.

Kwa nini sisi tushindwe?

Kwa nini msikiti usijue kuwa una madaktari wangapi, walimu wangapi, wajasiriamali wangapi na vijana wangapi wenye ujuzi mbalimbali?

Kwa nini utaalamu huo usiwe mtaji wa jamii?

Tunahitaji viongozi wenye maono na wanaoaminika

Lakini kuunganisha nguvu hizi kunahitaji aina maalumu ya uongozi.

Tunawahitaji viongozi wenye maono na uaminifu.

Kimoja kikikosekana, safari inakuwa ngumu.

Kiongozi anaweza kuwa mwaminifu sana, lakini kama hajui tunakwenda wapi, watu watabaki mahali pamoja. Anaweza pia kuwa na mawazo makubwa, lakini kama watu hawamwamini, hawatampa muda wao, utaalamu wao wala mali zao.

Maono ndiyo yanayosema: Tuna shule moja leo; ndani ya miaka 10 tujenge mtandao wa shule bora.

Maono yanaweza kusema: Badala ya kusaidia wagonjwa mmoja mmoja pekee, kwa nini tusijenge huduma ya afya yenye manufaa kwa maelfu?

Uaminifu nao ndiyo unaomfanya mfanyabiashara aseme: "Niko tayari kuchangia." Mtaalamu aseme: "Nitatoa ujuzi wangu." Kijana aseme: "Nitatoa muda wangu."

Hapo ndipo umma unapoanza kuwa timu.

Zakat na wakfu vinaweza kufanya makubwa

Uislamu tayari umetupatia zana za kujenga jamii.

Tuna zakat. Tuna sadaka. Tuna wakfu. Tuna utaalamu wa watu. Tuna muda wao. Tuna ardhi, biashara na mitandao.

Kinachohitajika ni kuvigeuza hivi kutoka juhudi zilizotawanyika kuwa nguvu iliyopangwa.

Fikiria wakfu uliosimamiwa kitaalamu kwa ajili ya elimu. Fikiria zakat inayoratibiwa vizuri kuwawezesha watu kutoka kwenye utegemezi kwenda kwenye uzalishaji. Fikiria wataalamu wa Kiislamu wakitoa saa chache kwa mwezi kusaidia miradi ya Umma.

Hayo si mambo ya kufikirika. Yanawezekana.

Lakini kama katika kuvuta kamba, lazima tuvute pamoja.

Tatizo letu huenda si ukosefu wa nguvu. Huenda nguvu zipo, lakini zimetawanyika.

Tunapozikusanya, kuzipanga na kuzielekeza katika maono yanayoaminika, ndipo vipaji vya watu binafsi vinageuka kuwa nguvu ya Umma.

Na hapo ndipo tutakapogundua kwamba pengine tulikuwa na timu nzuri muda wote — tulichokuwa tunakosa ni mfumo wa kuichezesha.

UONGOZI
UTAWALA

NA UKHTI FATIMA SS
0789 201 383

Kiongozi, jenga utamaduni huu ofisini kwako, utanishukuru

Mfanyakazi mzuri haondoki kazini kwa sababu ya mshahara pekee. Wakati mwingine anaondoka kwa sababu ya mazingira yanayomchosha, kutothaminiwa, upendeleo au uongozi usiosikiliza. Ndiyo maana moja ya kazi kubwa ya kiongozi si kusimamia watu tu, bali kujenga utamaduni ambao watu wanataka kubaki ndani yake.

Taasisi inaweza kuwa na ofisi nzuri, mishahara mizuri na jina kubwa, lakini kama wafanyakazi wanaingia kazini kwa hofu, kukata tamaa au kujiona hawathaminiwi, kuna tatizo. Utamaduni wa taasisi haujengwi na kauli mbiu iliyowekwa ukutani. Unajengwa na namna watu wanavyotendewa kila siku.

Kiongozi anayejenga taasisi imara anapaswa kujiuliza: Watu wangu wanajisikiaje wanapokuja kazini?

Tanguliza utu, si kazi pekee

Taasisi ipo kwa ajili ya kutimiza malengo, lakini malengo hayo yanatekelezwa na watu.

Kiongozi mzuri anajua kwamba mfanyakazi si mashine. Ana familia, afya, changamoto na matarajio ya maisha.

Hii haimaanishi kupunguza uwajibikaji. Inamaanisha kujenga mazingira ambayo yanamfanya mtu aweze kufanya kazi vizuri bila kuvunjwa na kazi hiyo.

Pale inapowezekana, kiongozi anaweza kuruhusu unyumbufu katika namna ya kufanya kazi, hasa kwa kazi ambazo si lazima mtu akae ofisini muda wote. Lakini hata pale ambapo uwepo kazini ni lazima, kuheshimu muda wa mapumziko na maisha binafsi ni muhimu.

Kufanya kazi hadi usiku kila siku si lazima iwe ishara ya taasisi inayofanya vizuri. Wakati mwingine ni ishara kwamba kazi haijapangwa vizuri.

Ondoa upendeleo

Moja ya vitu vinavyoweza kuua moyo wa timu haraka ni upendeleo.

Wafanyakazi wakiona mtu anapewa nafasi, sifa, safari, mafunzo au upendeleo mwingine kwa sababu ya ukaribu na kiongozi badala ya uwezo na kazi yake, uaminifu huanza kupotea.

Kiongozi anatakiwa kuwa na viwango vinavyoeleweka na kuvitumia kwa watu wote.

Hata kama huwezi kuwafanya watu wote wafurahie kila uamuzi, wanaweza kuheshimu uamuzi ikiwa wanaona umetolewa kwa haki.

Wape watu nafasi ya kusema

Katika baadhi ya taasisi, kiongozi ndiye anayesema na wengine wanasikiliza.

Huo si uongozi wenye afya.

Mfanyakazi wa chini anaweza kuona tatizo ambalo meneja wa juu halioni. Anaweza kuwa na wazo linaloweza kupunguza gharama, kuongeza wateja au kuboresha huduma.

Kama wafanyakazi wanaogopa kutoa maoni kwa sababu watadharauliwa au kuonekana wapinzani, taasisi inapoteza akili nyingi ilizoajiri. Kiongozi bora hasikilizi pongezi pekee. Anajenga mazingira ambayo mtu anaweza kusema, "Nadhani tunaweza kufanya hivi vizuri zaidi," bila kuogopa.

Thamini kazi nzuri

Watu wanahitaji kujua kwamba juhudi zao zinaonekana.

Si kila pongezi inahitaji fedha. Wakati mwingine "umefanya kazi nzuri," kutaja mchango wa mtu kwenye kikao au kumpa nafasi mpya kwa sababu ameonyesha uwezo kunaweza kuleta nguvu kubwa.

Tatizo ni pale ambapo makosa yanaonekana mara moja, lakini kazi nzuri inapita kimya kimya.

Kama unataka tabia nzuri ijirudie, itambue.

Pamoja na pongezi, wafanyakazi wanahitaji pia kuona njia ya kukua. Mafunzo, majukumu mapya, ushauri na nafasi za kupanda vyeo vinawafanya waone kwamba taasisi haiwatumii tu; inawajenga.

Usiruhusu 'tabiasumu' kazini

Kuna tabia ambazo kiongozi hapaswi kuzifumbia macho: kudhalilisha wengine, vitisho, kejeli, unyanyasaji, majungu yanayoharibu kazi na matumizi mabaya ya madaraka.

Mfanyakazi mwenye uwezo mkubwa lakini anayewavunja moyo wengine anaweza kuwa gharama kubwa kuliko faida anayozalisha.

Utamaduni mzuri unahitaji kuheshimiana.

Watu wanapaswa kujisikia salama kuwa wao wenyewe, kutoa mawazo yao na kufanya kazi bila kuogopa kudhalilishwa.

Punguza mikutano isiyo na lazima Si kila tatizo linahitaji kikao.

Taasisi nyingine zimejaa mikutano kiasi kwamba watu hawapati muda wa kufanya kazi waliyoajiriwa kufanya.

Kabla ya kuitisha kikao, kiongozi ajiulize: Je, jambo hili lingeweza kutatuliwa kwa simu, ujumbe au maelekezo mafupi? Mikutano michache lakini yenye malengo ni bora kuliko ratiba iliyojaa vikao visivyozalisha maamuzi.

NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383

Malezi rika kwa rika

SEHEMU YA 2

Miaka 3-5: Muda wa kumjengea mapenzi ya dini

Miaka mitatu hadi mitano ni kipindi cha maswali mengi, kuiga, kucheza na kutaka kujaribu kila kitu.

Mtoto wa umri huu anaweza kukufuata unapokwenda kuswali, akataka mswala wake, akajaribu kuinua mikono kama wewe na hata kurudia maneno anayokusikia ukisema.

Hapo mzazi ana nafasi kubwa sana. Badala ya kuanza kwa kumtwisha mtoto maelekezo mengi ya dini, anza kwa kumfanya aipende dini, aione nyumbani na aihusishe na furaha, upendo na usalama.

Watoto wa umri huu hujifunza sana kupitia kuona, kuiga, kucheza na kufanya mambo wenyewe. Kadiri wanavyokua, pia huanza kuwa huru zaidi, kuuliza maswali mengi na kuvutiwa zaidi na watu na mazingira yanayowazunguka. Kwa hiyo, malezi ya dini katika umri huu yanahitaji matendo mengi kuliko mihadhara.

Mruhusu mtoto asimame pembeni yako unaposwali. Mpe mswala wake mdogo kama inawezekana. Akifanya rukuu vibaya au akakimbia kabla swala haijaisha, usifanye kila kosa kuwa somo refu. Bado anajifunza.

Lengo la kwanza si kumfanya mtoto wa miaka minne aswali kama mtu mzima. Ni kumfanya aone swala kuwa sehemu nzuri na ya kawaida ya maisha yake.

Dini iishi ndani ya nyumba

Dua nazo zinaweza kufundishwa kwa njia hiyo hiyo.

Badala ya kumkalisha na kumpa orodha ya dua za kukariri, ziunganishe na maisha yake. Akianza kula, semeni Bismillah. Akimaliza, Alhamdulillah. Anapoingia nyumbani, mzoeshe kutoa salamu. Wakati wa kulala, soma naye dua.

Kurudia huku kwa kawaida kunaweza kujenga mazoea bila mtoto kuhisi yuko darasani kila wakati.

Hadithi pia zina nguvu kubwa katika umri huu. Mtoto tayari anaanza kukumbuka sehemu za simulizi na kufurahia hadithi zinazorudiwa.

Msimulie kuhusu Nabii Nuh, Ibrahim, Musa, Yusuf na Mitume wengine kwa lugha rahisi. Usijaribu kuingiza kila undani. Chagua jambo moja analoweza kuelewa: kusema kweli, kuwa na subira, kumtii Allah, kuwa jasiri au kuwasaidia wengine.

Baada ya hadithi unaweza kuuliza: "Umejifunza nini?" au "Tunawezaje kufanya jambo jema kama hilo leo?" Hapo dini inaanza kuingia katika maisha yake, si kichwani tu.

Mfundishe kwa kufanya

Mtoto wa miaka 3–5 anahitaji pia nafasi ya kufanya mambo. Mruhusu akusaidie kupanga vitu, kukusanya vitu vyake vya kuchezea, kuweka nguo mahali pake au kushiriki kazi ndogo zinazolingana na umri wake.

Hii si kazi tu. Ni malezi ya uwajibikaji.

Unaweza pia kumpa sarafu au fedha ndogo aiweke mwenyewe katika kisanduku cha sadaka au amkabidhi mhitaji. Hapo anaanza kuona kwamba kutoa si neno analolisikia, bali ni jambo analoweza kulifanya.

Vivyo hivyo Ramadhani isiwe mwezi ambao mtoto anakumbuka zaidi kwa kuambiwa: "Usile hiki," "usiingie hapa" au "kaa kimya."

Mfanye auone kwa upande wa furaha yake: futari pamoja, kusikiliza Qur'an, kwenda msikitini inapowezekana, kusaidia kuandaa chakula na kushiriki kutoa.

Usitafsiri kila ukaidi kuwa uasi

Mtoto wa miaka minne bado anajifunza kudhibiti hasira, tamaa na hisia zake. Anaweza kulia kwa nguvu kwa jambo ambalo mtu mzima anaona ni dogo. Anaweza kukataa, kurudia kosa au kubadilika ghafla kutoka furaha kwenda hasira.

Hii haimaanishi kwamba mzazi aache kuweka mipaka. Mipaka inahitajika, lakini iwe wazi, rahisi na thabiti. Badala ya kusema tu, "Usifanye hivyo," mwonyeshe anachotakiwa kufanya: "Haturushi vitu. Viweke hapa."

Badala ya kumpa machaguo mengi, mpe mawili rahisi: "Unataka kuvaa hiki au kile?" Hilo humsaidia kujifunza kufanya maamuzi bila kupewa uhuru unaozidi umri wake.

Na utalazimika kurudia. Mara nyingi sana. Malezi ya umri huu hayaendi kwa kusema jambo mara moja na kutarajia mtoto amelielewa milele.

NA UKHTI FATIMA SS
0789 201 383

Zijue njia 20 za ufundishaji

Mwalimu anaweza kuwa na maarifa mengi, lakini kama hajui namna nzuri ya kuyafikisha kwa wanafunzi, sehemu ya maarifa hayo inaweza isipate matokeo yaliyokusudiwa. Hizi hapa ni njia 20 zilizojaribiwa na kuleta matunda.

Mhadhara (lecture)

Mwalimu hueleza mada moja kwa moja kwa wanafunzi. Ni njia inayofaa hasa unapohitaji kutoa taarifa nyingi kwa kundi kubwa kwa muda mfupi. Hata hivyo, mhadhara pekee unaweza kuwafanya wanafunzi kuwa wasikilizaji tu, hivyo ni vizuri kuuchanganya na maswali au shughuli nyingine.

Majadiliano (Discussion)

Mwalimu na wanafunzi hubadilishana mawazo kuhusu mada. Njia hii huwafanya wanafunzi kufikiri, kuuliza maswali, kusikiliza mitazamo ya wengine na kujenga uwezo wa kujieleza.

Maonesho (Demonstration)

Badala ya kueleza tu jinsi jambo linavyofanyika, mwalimu analifanya mbele ya wanafunzi. Somo la sayansi, ufundi, mapishi au matumizi ya kifaa fulani linaweza kueleweka vizuri zaidi kwa kuoneshwa kuliko kuelezwa kwa maneno pekee.

Mradi (Project)

Wanafunzi hupewa kazi inayowataka kukusanya taarifa, kupanga na kutengeneza jambo fulani. Kwa mfano, wanaweza kufanya utafiti kuhusu uchafuzi wa mazingira katika eneo lao na kupendekeza suluhisho.

Semina (Seminar)

Mada huwasilishwa na kujadiliwa kwa kina. Njia hii inafaa zaidi kwa wanafunzi waliokomaa kiasi na inaweza kuwafundisha kutafuta taarifa na kuzitetea hoja zao.

Kongamano la wataalamu (Symposium)

Watu kadhaa wenye maarifa kuhusu eneo fulani hutoa mitazamo yao kuhusu mada moja. Wanafunzi hupata nafasi ya kuona kwamba jambo moja linaweza kutazamwa kutoka pande tofauti.

Warsha (Workshop)

Hapa wanafunzi hujifunza kwa kufanya. Badala ya kusikia tu kuhusu uandishi wa habari, kwa mfano, wanaweza kuandika habari; badala ya kuzungumzia upigaji picha, wapige picha.

Mdahalo wa jopo (Panel discussion)

Kundi dogo hujadili mada mbele ya wengine. Njia hii inaweza kufaa katika masuala yenye mitazamo tofauti, kama matumizi ya teknolojia shuleni au athari za mitandao ya kijamii.

Igizo (Role play)

Wanafunzi hupewa nafasi za kuigiza hali halisi. Mwanafunzi anaweza kuwa daktari, mgonjwa, mwandishi wa habari, mfanyabiashara au kiongozi. Igizo hujenga kujiamini, mawasiliano na uwezo wa kuelewa hali kutoka upande wa mwingine.

Kuchangia mawazo kwa wingi (brainstorming)

Mwalimu hutaja tatizo, kisha wanafunzi hutoa mawazo mengi kadiri wanavyoweza bila kuyahukumu mara moja. Baadaye ndipo mawazo hayo hupangwa na kuchambuliwa. Njia hii huchochea ubunifu.

Utatuzi wa matatizo (Problem-Solving)

Wanafunzi hupewa tatizo halisi au la kufikirika na kutafuta suluhisho. Badala ya kukariri majibu, wanajifunza namna ya kufikiri mpaka kufikia jibu.

Ugunduzi (Heuristic)

Mwalimu hatoi jibu moja kwa moja. Anawaongoza wanafunzi kufanya uchunguzi na kugundua maarifa wenyewe. Njia hii inaweza kujenga udadisi na uwezo wa kujifunza kwa kujitegemea.

Kutoka mifano kwenda kanuni (Inductive)

Wanafunzi hupewa mifano kadhaa, kisha wanasaidiwa kugundua kanuni inayoiunganisha. Kwa mfano, wanaweza kuchunguza sentensi mbalimbali kabla ya kufikia kanuni ya sarufi inayotumika.

Kutoka kanuni kwenda mifano (Deductive)

Hapa mwalimu huanza kwa kueleza kanuni, halafu wanafunzi huiona ikitumika katika mifano mbalimbali. Njia hii inafaa pale ambapo mwanafunzi anahitaji kwanza msingi wa kuelewa jambo.

Kazi za kufanya (Assignment)

Wanafunzi hupewa kazi za darasani au nyumbani zinazowataka kutumia maarifa waliyofundishwa. Kazi nzuri haipaswi kuwa adhabu, bali nafasi ya kufanya mazoezi na kujifunza kwa kujitegemea.

Mafunzo ya mtu mmoja au kundi dogo (Tutorial)

Mwalimu hufanya kazi kwa karibu zaidi na mwanafunzi au wanafunzi wachache. Njia hii inaweza kusaidia hasa pale wanafunzi wanapotofautiana katika kasi ya kuelewa.

Maabara (Laboratory)

Wanafunzi hujifunza kwa kufanya majaribio na kuchunguza matokeo. Ni muhimu sana katika sayansi, lakini dhana yake inaweza kutumika pia katika mafunzo mengine yanayohitaji vitendo.

Ufundishaji wa pamoja (Team teaching)

Walimu wawili au zaidi hushirikiana kufundisha somo moja. Kila mmoja anaweza kuleta utaalamu wake na hivyo kulifanya somo kuwa pana na lenye mitazamo tofauti.

Ufundishaji wa hatua kwa hatua (Programmed Instruction)

Maudhui hugawanywa katika hatua ndogo, mwanafunzi anamaliza moja kabla ya kuendelea na nyingine na hupata mrejesho katika kila hatua. Teknolojia za elimu zimeifanya njia hii iwe rahisi zaidi.

Ufundishaji wa mazoezi (Micro Teaching)

Mwalimu, hasa anayejifunza taaluma ya ualimu, hufundisha sehemu ndogo ya somo kwa muda mfupi ili kufanya mazoezi ya stadi fulani, kisha hupata mrejesho na kuboresha.

Somo kubwa hapa si kwamba mwalimu achague mojawapo ya njia hizi na kuitumia kila siku. fundishaji bora mara nyingi ni mchanganyiko. Mwalimu anaweza kuanza kwa maelezo mafupi, akaonesha mfano, wanafunzi wakajadili, halafu wakafanya kazi ya vitendo.

Swali la msingi halipaswi kuwa, “Ni njia gani ninapenda kufundishia?” bali, “Ni njia gani itawasaidia wanafunzi hawa kujifunza jambo hili vizuri zaidi?”

Kwa sababu mwisho wa siku, kipimo cha ufundishaji mzuri si kiasi ambacho mwalimu amezungumza — ni kiasi ambacho mwanafunzi ameelewa, anaweza kukumbuka na, muhimu zaidi, anaweza kutumia.

ربيع أول

TUJIFUNZE
AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama

Unawezaje kutumia AI kujipatia kipato?

SEHEMU YA 2

Bidhaa za Kielektroniki; Tengeneza mara moja, uza mara nyingi

Katika makala iliyopita tuliona kuwa unaweza kutumia akili unde (AI) kutoa huduma na kulipwa. Lakini kuna njia nyingine rahisi: kutengeneza bidhaa ya kidijitali na kuiuza kwa watu wengi.

Bidhaa ya kidijitali ni kitu ambacho mteja anakipokea kupitia simu au kompyuta badala ya kukabidhiwa bidhaa mkononi. Inaweza kuwa kitabu kidogo cha PDF, ratiba, kiolezo, mafunzo ya video, maswali ya kujifunzia au mwongozo wa kufanya jambo fulani.

Faida yake ni kwamba unaweza kuitengeneza mara moja na kuiuza zaidi ya mara moja. Kwa mfano, badala ya kumtengenezea mtu mmoja mpango wa bajeti kwa Sh10,000, unaweza kuandaa kiolezo kizuri cha bajeti na kukiuza kwa watu 50 kwa Sh3,000 kila mmoja.

Hapo ndipo AI inaweza kukusaidia.

Anza na tatizo, si AI

Usifungue AI na kusema tu: “Nipe bidhaa ya kuuza.” Anza kwa kuangalia watu wanaokuzunguka. Wanafunzi wanahangaika na nini? Wafanyabiashara wadogo wanahitaji nini? Wazazi wana tatizo gani? Watu wa taaluma yako wanapoteza muda kufanya jambo gani?

Kwa mfano, unaweza kugundua kuwa wauza nguo wengi wanaohudumia wateja kupitia WhatsApp hawajui namna ya kuweka kumbukumbu rahisi za mauzo.

Hapo unaweza kutumia AI kukusaidia kutengeneza daftari la kidijitali la mauzo, matumizi na faida linaloweza kutumiwa kwenye Excel au Google Sheets. Hiyo tayari ni bidhaa.

Tengeneza kitabu kidogo chenye msaada wa AI

Tuseme wewe ni mpishi mzuri. Unaweza kutengeneza mwongozo uitwao Mapishi 20 Rahisi ya Chakula cha Familia kwa Bajeti Ndogo.

Unaipa AI mawazo yako ya mapishi. Inaweza kukusaidia kuyapanga, kuandika orodha ya mahitaji, kurahisisha maelezo na kupanga sura. Baada ya hapo, wewe unakagua. Unaondoa makosa. Unaongeza uzoefu wako. Unaweka picha zako kama unazo. Kisha unaipanga vizuri na kuihifadhi kama PDF.

Violezo vinaweza kuwa biashara

Watu wengi hawataki kuanza kila kitu kutoka sifuri. Wanataka kitu kilichoandaliwa tayari.

Hapo ndipo violezo (templates) vinapokuwa bidhaa.

Mtu anayejua biashara anaweza kutengeneza kiolezo cha kutunza mapato na matumizi ya duka. Mwalimu anaweza kutengeneza ratiba za kusoma na mazoezi ya watoto. Mtaalamu wa ajira anaweza kuandaa violezo vya wasifu wa kazi (CV).

Mtu anayefahamu mitandao ya kijamii anaweza kutengeneza mpango wa siku 30 wa machapisho kwa saluni, mgahawa au duka la nguo.

AI inaweza kusaidia kutoa mawazo, kupanga yaliyomo na kuandika rasimu. Canva au Word inaweza kusaidia kuifanya bidhaa ionekane vizuri.

Ujuzi wako unaweza kuwa kozi ndogo

Huhitaji kutengeneza kozi yenye video 50. Kama unajua kupiga picha nzuri kwa simu, unaweza kuandaa video tano fupi: mwanga katika upigaji picha, ijue kamera, mbinu za upigaji picha, kuhariri na kuchapisha picha mitandaoni.

Fundi cherehani anaweza kufundisha vipimo vya msingi. Mhasibu anaweza kufundisha namna ya kutenganisha fedha ya biashara na fedha binafsi. Mkulima anaweza kuandaa mwongozo wa jambo analolijua vizuri.

AI inaweza kukusaidia kupanga masomo na kuandika muhtasari. Lakini haiwezi kuchukua nafasi ya maarifa ambayo huna.

Usitengeneze kwanza, ndipo utafute mnunuzi

Hili ndilo kosa kubwa. Kabla hujaandika kurasa 50, waulize watu 10 unaowalenga: “Kitu gani kinakusumbua zaidi kuhusu kutunza fedha za biashara?” Majibu yao yanaweza kukuonyesha bidhaa wanayohitaji.

Anza na kitu kidogo. Kiuze. Sikiliza maoni. Kiboreshe.

AI imefanya kutengeneza bidhaa za kidijitali kuwa rahisi zaidi. Lakini biashara bado inaanza pale pale ilipoanza siku zote: kutatua tatizo la mtu.

Usijiulize tu, “AI inaweza kunitengenezea nini?” Jiulize: “Ni tatizo gani ninaweza kusaidia kulitatua, halafu AI inanisaidiaje kulitatua haraka na vizuri zaidi?” Hapo ndipo faili la kawaida linaweza kuanza kuwa bidhaa — na bidhaa ikaanza kuwa chanzo cha kipato.

Ukishatengeneza, unauza wapi?

Huhitaji kuwa na tovuti kubwa ili kuanza. Tanzania unaweza kuanzia WhatsApp, Instagram, Facebook au Telegram kwa kutangaza bidhaa yako kwa watu wanaoweza kuihitaji. Mteja akivutiwa, anaweza kulipa kwa M-Pesa, Airtel Money, Mixx by Yas au benki, kisha ukamtumia bidhaa kwa WhatsApp, barua pepe au kiungo cha kupakua.

Kwa mfano, ukiwa umetengeneza kiolezo cha bajeti ya biashara, unaweza kukitangaza kwenye makundi ya wafanyabiashara WhatsApp au Facebook. Ukiwa na mwongozo wa mapishi, unaweza kutumia Instagram, TikTok au WhatsApp Status kufikia wateja.

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama

Tabia ndogo za kila siku zinazoweza kuathiri afya yako

Magonjwa mengi sugu hayaanzi kwa tukio moja kubwa. Mara nyingi hatari hujengwa taratibu kupitia mambo tunayofanya kila siku — tunavyokula, tunavyokaa, tunavyolala na hata tunavyotumia muda wetu.

Habari nzuri ni kwamba baadhi ya tabia hizi zinaweza kubadilishwa bila gharama kubwa.

Si sahihi kusema kwamba tabia moja pekee ndiyo "inasababisha" kisukari, shinikizo la damu, ugonjwa wa moyo au matatizo ya figo. Magonjwa haya huwa na visababishi vingi, vikiwamo urithi, umri na hali nyingine za kiafya. Lakini tabia za maisha zinaweza kuongeza au kupunguza hatari.

Kukaa muda mrefu bila kufanya mazoezi

Leo watu wengi wanafanya kazi wakiwa wamekaa, wanatumia magari kwa safari nyingi na muda wa mapumziko unakwenda kwenye televisheni au simu.

Mwili haukuumbwa ukae siku nzima.

Kutofanya shughuli za mwili huongeza hatari ya magonjwa ya moyo, kisukari aina ya pili, shinikizo la damu na kuongezeka uzito. Hata kutembea kwa kasi, kufanya kazi za nyumbani au kutumia ngazi kunaweza kusaidia. WHO inapendekeza watu wazima kupata angalau dakika 150 za shughuli za mwili za kiwango cha wastani kwa wiki.

Chumvi nyingi kwenye chakula

Chumvi inaweza kuonekana jambo dogo, lakini kuitumia kupita kiasi huongeza shinikizo la damu na hivyo kuongeza hatari ya magonjwa ya moyo na kiharusi.

Tatizo si chumvi tunayoongeza mezani pekee. Inaweza pia kuwa nyingi katika baadhi ya vyakula vilivyosindikwa, vitafunwa na viungo vya kupikia.

WHO inapendekeza mtu mzima kutumia chini ya gramu tano za chumvi kwa siku — takribani kijiko kimoja cha chai kwa jumla kutoka kwenye vyakula vyote.

Kulala mara tu baada ya kula

Kula chakula kingi halafu kujilaza mara moja kunaweza kuongeza tatizo la tindikali ya tumboni kurudi kwenye umio, hasa kwa watu wenye tatizo hilo tayari.

Kwa mwenye dalili za kiungulia au tindikali kurudi mdomoni, wataalamu wanashauri kula angalau saa tatu kabla ya kulala.

Kwa hiyo, chakula kizito cha usiku halafu moja kwa moja kitandani si utaratibu mzuri, hasa kama unapata kiungulia mara kwa mara.

Kula kwa haraka sana

Kuna watu wanamaliza sahani ndani ya dakika chache.

Kula haraka hakumaanishi moja kwa moja kwamba utapata gastritis, kama baadhi ya ujumbe wa mitandaoni unavyodai. Lakini kunaweza kukufanya ule zaidi kabla mwili haujapata muda wa kutambua kwamba umeshiba, na baadhi ya watu hupata usumbufu wa tumbo.

Polepole. Tafuna vizuri. Chakula si mashindano.

Kutokunywa maji ya kutosha

Maji yanahitajika katika shughuli nyingi za mwili. Kutokunywa maji ya kutosha kunaweza kuongeza uwezekano wa kukosa choo vizuri, na kwa baadhi ya watu kunaweza kuchangia kutokea kwa mawe kwenye figo.

Lakini hakuna kiwango kimoja cha maji kinachofaa kila mtu. Mahitaji hutegemea hali ya hewa, shughuli unazofanya, chakula na afya yako.

Katika mazingira ya joto kama Tanzania, hasa kwa anayefanya kazi nzito au mazoezi, kupuuzia kiu si jambo jema.

Chai mara baada ya chakula?

Kwa Watanzania wengi, chai ni sehemu ya maisha.

Lakini chai ina kemikali zinazoweza kupunguza ufyonzwaji wa madini ya chuma yanayotokana hasa na vyakula vya mimea. Hili linaweza kuwa muhimu zaidi kwa watu walio katika hatari ya upungufu wa madini ya chuma.

Hii haimaanishi chai ni mbaya. Ni suala la muda na kiasi.

Usisubiri ugonjwa ndipo ubadilike

Afya nzuri haijengwi kwa uamuzi mmoja mkubwa wa Januari.

Inajengwa na maamuzi madogo yanayorudiwa: kutembea zaidi, kupunguza chumvi, kula kwa utulivu, kunywa maji, kupata usingizi wa kutosha na kutokulala mara baada ya chakula.

Na kama una dalili zinazoendelea — kiungulia kikali, uchovu usioelezeka, maumivu, shinikizo la damu au dalili nyingine — usitegemee ushauri wa mitandaoni pekee. Muone mtaalamu wa afya.

Tabia ndogo zinaweza kuonekana hazina maana leo. Lakini zinaporudiwa kwa miaka, zinaweza kuwa uwekezaji katika afya yako — au deni ambalo mwili utakuja kulidai.

UKHTI FATIMA SS

Tabia saba ndogo lakini kikwazo cha mafanikio yako

Wakati mwingine kinachomzuia mtu kusonga mbele si ukosefu wa kipaji, fedha au fursa. Ni tabia ndogo anazozifanya kila siku mpaka zinakuwa sehemu ya maisha yake.

Mwandishi Colby Kultgen anaziita baadhi ya tabia hizo "addictions" — aina ya utegemezi unaoweza kumfanya mtu ashindwe kutumia uwezo wake kikamilifu. Si zote ni uraibu kwa maana ya kitabibu, lakini hoja yake ni kwamba tabia zikijirudia kwa muda mrefu zinaweza kutawala muda, fikra na maamuzi yetu.

Anazitaja saba: kujilinganisha, kukata tamaa, kusubiri mazingira kamili, kuzama kwenye simu, kuahirisha mambo, kujifanya mwenye shughuli nyingi na kuogopa kutoka katika eneo la mazoea.

Kujilinganisha na wengine

Mitandao ya kijamii imerahisisha kujilinganisha. Unaona mwenzako amenunua gari, mwingine amejenga nyumba na mwingine amepandishwa cheo. Unasahau kwamba unaangalia sehemu ndogo tu ya maisha yao.

Tatizo la kulinganisha maisha yako na ya wengine ni kwamba unaweza kuharakisha malengo yasiyo yako, kukosa kuridhika na ulipo na kujiona hufai.

Badala yake, jilinganishe zaidi na ulivyokuwa jana. Kujifunza kushukuru kwa kile ulicho nacho hakumaanishi kuacha kutamani maendeleo; kunasaidia kuhakikisha hutumii maisha yako kuendesha mbio ambazo hukuzichagua.

Kukata tamaa mapema

Kuna tofauti kati ya kuacha jambo lisilofaa na kukimbia kila jambo linapokuwa gumu.

Malengo mengi huhitaji muda mrefu kabla matokeo hayajaonekana. Biashara inaweza kuchelewa kupata wateja, mwanafunzi anaweza kutofanya vizuri mwanzo na mtu anayejifunza ujuzi mpya anaweza kujiona hana kipaji.

Kukata tamaa mara tu baada ya kushindwa kunakata pia uwezekano wa kujifunza kutokana na kosa. Wakati mwingine kinachohitajika si kuacha lengo, bali kubadili mbinu.

Kusubirisha kuanzisha jambo hadi ukamilifu "Nitaanza nikipata fedha." "Nitaandika nikiwa na muda." "Nitaanzisha biashara nikishakuwa tayari." Tatizo ni kwamba mazingira kamili mara nyingi hayaji.

Wakati mwingine watu wenye ujuzi mdogo hututangulia kwa sababu moja rahisi: wameanza. Hii haimaanishi kufanya maamuzi bila maandalizi, bali kutokuruhusu hofu iliyojificha katika jina la "maandalizi" ikuzuie kuchukua hatua.

Ukisubiri kuwa tayari kimaandalizi kwa asilimia 100, unaweza kusubiri milele. Waswahili husema mwanzo mgumu.

Uraibu wa simu

Dakika tano za kuangalia simu zinaweza kugeuka dakika 30. Dakika 30 kila siku zinaweza kuwa mamia ya saa kwa mwaka. Tatizo si simu yenyewe. Simu ni chombo muhimu cha kazi, elimu na mawasiliano. Tatizo ni tabia ya kuendelea kusogeza skrini bila kusudi—scrolling—ambayo inaweza kula muda ambao ungeweza kutumika kusoma, kufanya kazi, kulala au kuzungumza na familia.

Njia moja rahisi ni kuweka nyakati ambazo simu haihusiki, hasa kabla ya kulala na baada ya kuamka.

Kuahirisha mambo

"Kesho" ni moja ya maneno hatari katika utekelezaji wa malengo. Tunapoahirisha kazi ngumu, mara nyingi si kwa sababu hatuna muda bali kwa sababu tunakwepa hisia zisizopendeza zinazohusiana nayo.

Mbinu rahisi ni kujiambia utafanya kazi hiyo kwa dakika tano tu. Mara nyingi sehemu ngumu zaidi si kazi yenyewe—ni kuanza.

Kuwa na shughuli nyingi bila maendeleo

Kuwa bize si sawa na kuwa na tija. Unaweza kujibu ujumbe, kuhudhuria mikutano, kupanga mafaili na kukimbia siku nzima, lakini mwisho wa siku usiwe umefanya jambo moja lenye kusogeza lengo lako mbele.

Jiulize kila jioni: Ni jambo gani moja nililofanya leo ambalo limenisogeza mbele? Swali hilo linaweza kutenganisha shughuli na maendeleo.

Kuogopa kutoka katika mazoea

Maeneo tunayoyazoea hutupa hali ya kujihisi salama. Lakini ukuaji mara nyingi huanza pale tunapojaribu jambo ambalo linatutoa katika mazingira tuliyoyazoea. Si lazima kuchukua hatari kubwa. Anza na changamoto ndogo: sema mbele ya watu, jifunze ujuzi mpya, omba nafasi, anzisha mradi au jaribu njia tofauti.

Mwisho wa yote, maisha hayaharibiwi tu na maamuzi makubwa mabaya. Wakati mwingine yanacheleweshwa na tabia ndogo zinazojirudia kwa miaka.

Na habari njema ni kwamba tabia zinaweza kubadilishwa.

Anza na moja.